DISEMBA MMXXIV-TOLEO LA XXXIX

# NGURUMO

*ya Mwandishi*




## PIGA HATUA...

## YALIYOMO

**TAHARIRI**— PIGA HATUA —Uk 02

**MWANDISHI WETU**— Kalmas Konzo — Uk 03

**New In Town:** — MSALITI na OPERESHENI KASHIMR— uk 04

**PITIO LA VITABU**— NGUZO MAMA—Uk 06

**MAKALA** — **SAIKOLOJIA**: Muoneshe Uhalisia —Uk 06 na 07

**MAKALA:** Vtabu Nilivyosoma 2024 uk 08

**MIAMBA WA AFRIKA:** PATRICE LUMUMBA '3'— Uk 10

**Sako kwa Bako**– Kindo Emmanuel —Uk 11

**RIWAYA:** — SHAJARA YA MUUAJI '10'—Uk 12 na 13

**RIWAYA—** Cronoc 7 '20'- Uk 14 na 15

**YA KALE NI DHAHABU**: — Alibaba na Wezi 40 '15'- Uk 16

**HABARI:** MKUKI NA NYOTA, Bingwa Katika Uchapaji – Uk 17

**SHUBAKA LA VITABU:** Vidokezo 35 Vya Usomaji Vitabu —Uk 18

**KITABU NILICHOSOMA:** The Power of Dicipline na From Mopping Floors —Uk 19

**MATANGAZO: -** Uk 20

**MALENGA WA KILEO:** MWAKA UMETUKIMBIA…— Uk 21

**HABARI PICHA: -** Uk 22

**KUTOKA MAKTABA:** Maisha ni Mapambano '6'-Uk 23

**ELIMU JAMII:** — USINGIZI —Uk 24

**HADITHI:** — Happy New Year '2' Uk. 26 na SHEMEJI USIZIME TAA…! '2'

—27

## TAHARIRI:
# 2025 PIGA HATUA

Salaam kwako mpendwa msomaji wa Ngurumo ya mwandishi. Najua una furaha sana kumaliza mwaka 2024 na kuuanza mwaka mpya wa 2025. Je; umetathmini mafanikio ya 2024 katika malengo yako uliyojiwekea? Je; umefanikiwa kiasi gani? Wapi umeshindwa? Kaa chini ujiulize yote hayo kisha yafanyie kazi katika mwaka huu mpya.

Mwaka 2025 piga hatua! Hatua katika nini? Hatua katika kufanikisha yale ambayo umejipangia. Je una utaratibu wa kupanga mipango ya kuitekeleza kila mwaka?

Kuishi bila mipango ni sawa na kuishi kama jiwe. Lakini wewe kama mwanadamu, yakupasa kuwa na mipango. Unataka kufika paleee… ndiyo. Lakini bila mipango utafikaje?

Rafiki, mwaka 2025 panga mpango mmoja au miwili tu mahususi ya kukutoa sehemu moja kwenda nyingine. Weka chini mikakati yako ya kuifanikisha mipango hiyo. Tia nia moyoni mwako kisha mshirikishe Mungu katika hiyo mipango. Halafu weka kwenye matekelezo kwa vitendo. Kila siku ya Mungu, jioni kabla ya kulala kaa chini jiulize, umefanya kwa kiasi gani…, kila mwezi unapoisha jiulize umefanya kwa kiasi gani, kama kuna eneo umeshindwa jiulize kwa nini umeshindwa, kisha mwezi unaofuata hakikisha lile uliloshindwa unalishinda.

Mimi nitakupa mbinu moja mahususi katika hilo, nayo ni 'KUSOMA VITABU". Soma vitabu vinavyofundisha maarifa ya maisha. Vipo vingi sana, vya Kiingereza kwa Kiswahili. Kama unapenda kuvijua basi wasiliana nami kwa whatsapp 0766974865, na vingine nitakupa kwa soft copy ujisomee, ujifunze, uweke katika matendo.

Nakuhakikishia, mpaka mwezi wa mwisho wa mwaka utapotathimini utakuta umefanikiwa zaidi ya 80%

Haya tuanze sasa…

CEO— *Richard Mwambe*

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

# MWANDISHI WETU:
## KALMAS KONZO

**Huwezi kupita facebook ukakosa kuona maandiko yake matatu kwa siku moja. Kalmas, kutoka Njombe ndiye mshindi nambari tano katika Tuzo Nyerere ya Uandishi Bunifu ya 2023.**

**Katika toleo hili, tumerudia mazungumzo yetu tuliyoyafanya naye miaka kadhaa nyuma, lakini kabla ya kuchapa tena tulimuuliza swali moja tu, 'kwanini huandika anayoyaandika katika facebook?' akatujibu...**



**Picture caption**

Naitwa Kalmas Konzo. Nimezaliwa Mafinga mkoani Iringa, lakini kwa sasa ninaishi mjini Njombe katika mkoa wa Njombe.

Historia yangu katika utunzi na uandishi wa hadithi imeanzia mbali sana. Wakati nikiwa mdogo nilikuwa napenda sana kusoma vitabu vya waandishi nguli kwa kipindi hicho hususani hadithi za kijasusi. Waandishi kama Elvis Aristablus Musiba, Ben Mtobwa, Hammie Rajab, John Simbamwene n.k walinijenga sana katika kupenda hadithi.

Nikiwa nasoma mimi na rafiki yangu bwana Fadhy Mtanga tulikuwa tukipeana hamasa kubwa sana katika utunzi na uandishi wa hadithi. Tulikuwa na ndoto za kuja kuwa waandishi wakubwa hapo siku za baadaye. Mwaka 2010 ndiyo nikaanza kutunga simulizi rasmi maana kipindi cha nyuma nilikuwa nikitunga kama sehemu ya burudani yangu.

Mpaka sasa nimefanikiwa kuchapisha kitabu kimoja kiitwacho LADHA YA KIFO. Mungu akijaalia mwishoni mwa mwaka huu nitaingiza sokoni vitabu vingine viwili.
Pia nina hadithi nyingi sana ambazo ziko katika mfumo wa nakala laini.

Instagram napatikana kama **@hadithi za konzo** na facebook napatikana kama **Simulizi za Konzo**.
Nawashukuru sana waandishi wenzangu wote kwani tumekuwa na ushirikiano mkubwa katika kubadilishana mawazo pamoja na kujengana.

Naawashukuru pia wapenzi wa hadithi zangu kwani siku zote wamekuwa pamoja nami na kuniunga mkono katika njia mbalimbali.

Mwisho nichukue fursa hii kuiomba jamii yote ya Watanzania kuamsha ari ya usomaji. Unaposoma, unaushibisha ubongo maarifa. Fanya vitabu kuwa ni sehemu ya bidhaa unazonunua mara kwa mara.

Ahsante sana uongozi wa jarida la NGURUMO YA MWAMNDISHI kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuweza kuonekana katika ukurasa huu. Mungu awabariki na niwatie moyo kwa hiki mnachokifanya.

***Kalmas, siku hizi za karibuni tumekuwa kila tukipita kwenye kuta za facebook, kwa siku moja tutakuta maandiko yako matatu au zaidi. Lakini maandiko au video hizo huwa ni burudani na utani uliokithiri. Hebu tuambie, kwanini unapenda kuandika unayoyaandika, au kuweka zile video unazoweka?***


Kwanza kabisa mimi napenda sana sanaa ya ucheshi. Pia mimi ni mtu wa furaha. Huwa napata amani ninapoona jamii yangu ina furaha. Watu huwa wanapatwa na msongo wa mawazo kutokana na shughuli zao za utafutaji kipato kutwa. Hivyo huwa wanahitaji burudani itakayopunguza msongo na kuwafanya wawe kawaida. Kwa hiyo machapisho yangu ya kufurahisha ni tiba ya fikra kisaikolojia. Zaidi na kubwa ni kwamba kwenye machapisho yangu huwa kunakuwa na ujumbe ambao huwa katika muktadha wa aidha kuponya, kuelimisha, kuburudisha, kutahadharisha, kukemea na kadhalika. Kwa sababu watu wanapenda burudani basi nami nikaona kwa njia hiyo naweza kuwafikishia ujumbe wanajamii.

# NEW IN TOWN :
# MSALITI na OPERESHENI KASHMIR

## MSALITI

MISITU ya Mashariki mwa Jamhuri ya Demokrasia ya Congo inaigeuza historia ya walinda amani wa Tanzania ndani dakika chache tu. Sheria ya Kimataifa inakiukwa, walinda amani wanashambuliwa na uhai unapotea huku wengine wakibaki na majeraha ya kutisha. Huzuni! Uchungu!
Mgogoro usiopatiwa ufumbuzi kati ya waasi wa CRA na jeshi la Congo DR unakuwa tatizo sugu katika Afrika na dunia. Kelele zinapigwa, majeshi yanaenda lakini bado hali ni ileile. Kuna nini?
Vifo vya wanajeshi wa Kitanzania vinaiibua TSA inayoongozwa na Madam S. chanzo cha yote ni simu iliyopigwa nyumbani kwa Kamanda Amata. Mpigaji kabla hajajitambulisha, simu ikakatika… alitaka kusema nini?
Hii ni riwaya nyingine ya ubunifu, inayouangazia mgogoro wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo katika mtindo bunifu. Hakika hiki ni moja ya kitabu ambacho hutokisahau maisha ni mwako.
Ni kalamu ileile ya *'Mmwela'* aliyebarikiwa.

Kitabu hiki kimeandikwa na Richard Mwambe…




## OPERESHENI KASHMIR

'PT - 502 - B. PEGAN X' Ndiyo chanzo cha yote. Mfumo maalum wa usalama uliopachikwa kwenye ndegevita mpya kabisa ya kisasa na ya kwanza Afrika unatikisa matajiri wanaomiliki maisha ya watu na kutengeneza pesa kwa kutoa roho zisizo hatia.

Serikali na Jeshi la Wananchi Tanzania wanafanya manunuzi ya ndegevita tatu zenye mfumo huo hatari wa kujilinda na kung'amua makombora achilia mbali kushambulia.


Lakini ndege hiyo inatekwa na wajuvi huku ndani yake ikiwa na makepteni watatu.

Huku Tanzania, kiza kinene kinatanda juu ya hilo. Vikao haviishi ili kujua hatima ya yote. TSA1 Kamanda Amata anafunga mjadala kwa kuingia msambweni. Anaanzia Dar es salaam, Zanzibar, Islamabad mpaka Kashmir.

Je nini huko kitajiri? Hii hapa OPERESHENI KASHMIR, kalamu ya *'Mmwela'* aliyebarikiwa.


**Vitabu hivi, vinapatikana**
**Dar es salaam,**

- **Duka la Kona ya Riwaya- Simu namba 0655248085**
- **Posta Mpya kwa George**



# NGUZO MAMA






**KITABU** – NGUZO MAMA

**MWANDISHI** – PENINA MHANDO

**WACHAPISHAJI** – DUP

**MWAKA** – 1982

**MHAKIKI:** MWALIMU MAKOBA

Tamthiliya ya Nguzo Mama inayazungumzia matatizo anayokutana nayo mwanamke na harakati anazofanya ili kujinasua. Wakati mitazamo mingine ikisema kuwa matatizo ya mwanamke yanasababishwa na jamii yake na mila potofu Penina mhando anakuja na dhana mpya, **"matatizo ya mwanamke yanasababishwa na mwanamke mwenyewe."**

**Maudhui**

**1. Dhamira**

**i. Ukombozi wa mwanamke**

Mwandishi anaonesha manyanyaso makali anayopewa mwanamke. Bi Pili anapigwa kila siku na mumewe, anafanya kazi lakini mumewe anachukua pesa yote inayopatikana. Suluhisho la matatizo haya na mengine yanayojitokeza ni kusimama kwa Nguzo Mama.

**ii. Uongozi mbaya**

Mwenyekiti anaongoza kwa mabavu. Anapelekewa kesi na Bi Nne. Bi Nne anamtuhumu Bi. Nane. Mwenyekiti kwa kutumia mabavu anatoa maamuzi pasipo kumsikiliza Bi. Nane. Udikteta kama huu, unachelewesha maendeleo ya mwanamke.

**iii. Elimu**

Ni vyema elimu itolewe kwa watu wote. Kukosekana kwa elimu ni sababu mojawapo inayochelewesha maendeleo Patata. Mfano Bi. Saba ambaye ni kiongozi wa kamati ya wanawake, hajui maana ya nguzo mama.

**iv. Umasikini**

Suala la umasikini ni tatizo sugu ambalo bado halijapatiwa dawa. Bi. Tano anaishi maisha magumu, hana pesa ya kuwanunulia nguo watoto wake, hana pesa ya kununulia chakula. Wanawake wanafanya harakati nyingi ili kuondokana na umasikini lakini bado tatizo hili linaendelea.

**v. Nafasi ya mwanamke katika jamii**

Mwanamke amechorwa kama,

- Chombo cha starehe

Bi. Sita anafanya biashara ya kuuza mwili, wanaume wanamnunua na kumtumia kwa kujistarehesha.

- Mwenye busara

Bi. Nane ana busara, yeye anawashauri wanawake wenzake wajishughulishe na miradi tofauti tofauti ili waweze kujikomboa kiuchumi.

- Kiumbe dhaifu na asiye weza kutoa maamuzi yoyote

Sudi anampiga mkewe Bi. Pili. Anapomaliza kumpiga, anachukua hela zake zote na kwenda kunywa pombe.

- Mama mlezi wa familia

Mwanamke amechorwa kama anayejishughulisha na mambo yote yahusuyo familia yake, yeye ndiye anayejua watoto wamekula nini na kama wako salama.

**2. Ujumbe**

i. Fimbo ya mnyonge ni umoja

Wanawake wanatakiwa kuungana ili kupambana na matatizo yanayowakabili, makundi na majungu hayana msaada.

ii. Ili jamii iendelee lazima kuwe na misingi ya uongozi bora

Mwenyekiti na Bi. Nne wanakwamisha maendeleo ya wanawake kwa sababu hawakuwa na misingi ya uongozi bora, ili jamii ijikwamue ni lazima suala hili liwekewe mkazo

***Uchambuzi huu utaendelea katika toleo lijalo...***

# -SAIKOLOJIA-

## MUONYESHE UHALISIA WAKO MWANZONI KABISA WA MAHUSIANO YENU

**Neema Mgao**

**WhatsApp +255763013206**

**Insta: neymgao**

**Facebook: NEEMA MBILINYI MGAO**



U hali gani ndugu yangu? heri ya CHRISTMASS NA MWAKA MPYA. Hakika Mungu ni mwema sana hata tumekutana tena katika toleo hili la mwezi Disemba. Ni toleo la mwisho kabisa kwa mwaka 2024.Yapo mambo mengi sana ambayo tumeyapitia kwa mwaka 2024, mengine yalizungumza na sisi kwa lugha laini ya kubembeleza na ya kuridhisha sana. Lakini utakubaliana na mimi kuwa yapo mengine magumu tuliyopitia ambapo kwa namna moja au nyingine yalitufanya tutoke kabisa kwenye mhimili wa imani zetu. Yote kwa yote, ikiwa upo hai, unapumua, iwe mambo hayaendi au yanaenda, mshukuru Mungu.

**MERRY CHRISTMASS AND HAPPY NEW YEAR.**

Katika toleo la mwezi huu nimetamani tuzungumze jambo nyeti na la umuhimu sana, jambo ambalo ni msingi wa mahusiano ambapo watu wengi sana kwenye jamii yetu tumeshindwa kabisa kuanza nalo mwanzoni kabisa mwa mahusiano mengi hivyo kupelekea kutokea kwa sintofahamu ya mabadiliko yale yaitwayo 'ya tabia'.

Mara nyingi sana, mahusiano yanapoanzishwa na wapendanao, huwa kunatokea kufichana mambo mengi ikiwemo tabia halisi za wapendanao hao. Mara nyingi sana, zile tabia watu walio kwenye mahusiano hasa yale ya mwanzoni kabisa huwa sio halisi. Takwimu za kisaikolojia zinasema, asilimia kubwa ya tabia za watu, takribani 75%, hasa pale wanapoanzisha mahusiano mapya huwa si tabia zao halisi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba tabia halisi zinapooneshwa kutakua na uwezekano mkubwa wa watu kuachana pengine siku ya tatu tu.

Lengo la andiko hili katika mwanzoni kabisa mwa mwaka ni kukueleza namna ya kufanya mahusiano yako yadumu kwa kutegemea uhalisia kabisa.

2025 utakapo anzisha mahusiano au ikiwa unahitaji kuboresha hayo mahusiano yako yaliyofikisha mwezi mmoja [*maana haujachelewa*] nakusihi, onyesha uhalisia wako ili mwenza wako aamue kipi akubadilishe au kipi akuongeze ili mwendane sawasawa katika maisha yenu ya mahusiano.

Kuuficha uhalisia imekua janga ambalo limepelekea wapenzi kuona kama kuna mabadiliko ya kitabia. Unaweza kushuhudia wapenzi wakishutumiana katika mabadiliko ya tabia, kwamba *"mpenzi wangu hakua na tabia hii"*, kwamba *"mwanzoni tulipoanza hakua hivi kabisa, imekuaje sasa?"*, na utakubaliana na mimi kuwa, unaweza kushuhudia huyo anayelalamikiwa pengine akawa anashangaa, kwamba *"huyu anasemaje kuwa nimebadilika? mbona mi mi nipo vilevile jamani?"*. Yeye hawezi kujiona kama amebadilika, kwani alivyoanza na wewe mwanzoni alikua katika kuigiza tabia alizonazo lakini ukweli ni kuwa hajabadilika, maana hakua yeye yule wa mwanzo, ilikua ni mbinu ya kukuteka ili uwe naye. Na ndio maana utaona mwanzoni kabisa, atakuuliza kuwa *"unataka mwanamke au mwanaume wa aina gani?* au *"unataka niweje"* na ukishasema vile unavyotaka awe, nae anakua hivyo hivyo, ni kwa sababu anataka uone kuwa *"hapa nimepata",* kumbe mmhh, uhalisia wake ni mtu mwingine kabisa, sasa akichoka kuigiza na akawa kwenye ule uhalisia wake kabisa ndio hapo utauona 'moto' kwenye mahusiano au ndoa hiyo.

Katika ndoa, yafaa wanandoa kuwekeana mipango mikakati mwanzoni kabisa mwa ndoa zao, kwamba mimi nimefunga ndoa na wewe na sio ndugu zako, hivyo ndugu zako ni ama wasikanyage kabisa hapa kwetu, au wakija, waje mwisho watatu kwa mwaka, na wasikae zaidi ya siku mbili. Au mwanamke mweleze mumeo kuwa, ingawa umenioa, mimi niko nafanya kazi hii na hii, hivyo pamoja na kuwa tunaigia kwenye maisha ya ndoa, kazi zangu nataka kuendelea nazo, na kwamba siku utakayotaka kuniachisha kazi mimi, basi mimi na wewe ndoa au mahusiano yetu yataishia hapo. Mtakapoambiana ukweli, mwanzoni kabisa

## MUONYESHE UHALISIA WAKO MWANZONI KABISA WA MAHUSIANO YENU

mwa mahusiano yenu, basi, inakua ni hiyari ya mwenza husika kuamua ama asuke au anyoe. Ukweli usemwe mwanzoni kabisa na wapenzi au wenza wauishi kabisa uhalisia na ukweli huo.

Yapo mahusiano na ndoa nyingi zimegeuka makaa ya moto kutokana na wanandoa kufichana uhalisia au mambo yao pindi wanapoyaanza. Nimeonelea leo katika toleo hili tuambizane jambo hili ambalo limeleta maafa sana katika jamii zetu. Jamii imeshuhudia ugomvi wa mara kwa mara kwa wapendanao kugombana wakishutumiana kubadilika kitabia. Baada ya uchunguzi na utafiti nilioufanya katika makundi mbali mbali ama ya wanandoa au ya wapenzi wa karibu, nikabaini jambo hili ambalo pia mimi na wewe tunaweza kuwa ni wahanga wa tabia hii ya kuficha uhalisia.

Mahusiano bila pesa haiwezekani, mwanamke usiigize kuvumilia kutokupewa pesa kwa minajili ya kuwa eti hujampendea pesa. Mwambie kabisa kuwa pamoja na kukupenda, na huduma zako, na pesa nazihitaji.

Hupendi mkeo afanye kazi mweleze mapema kabla hamjaingia kwenye ndoa. Kwamba nikikuoa nataka utulie tu nyumbani, usifanye kazi yoyote.

Unapenda kubembelezwa na kudekezwa pamoja ya kuwa wewe ni mwanaume, usijivunge, raha tupate wote.

Hupendi ashike simu yako mweleze, simu ni kwa ajili ya mawasiliano binafsi. Simu zimeparanganisha sana wapendanao, unashika simu ya mwanamke au mwanaume wako ya nini? Kila mmoja si yupo na simu yake, tumia yako. Sasa akikwambia kuwa usishike simu yake umuelewe, sio kuanza uchunguzi na kupindisha macho yakawa macho *kumchuzi* huku mkono *kudagaa.* Kama huwezi mwache aende, wapo wanaoweza wakakaa na simu ya mke au mume hapo karibu na bado wasiiguse.

Kwamba wewe mapenzi bila kinyume na maumbile haujaridhika bado{*jinsi zote mbili, me na ke*}, yaani kwamba wewe ni wale waliomchoka Mungu, iwe ni mwanamke au ni mwanaume, kwamba wewe ni firauni kama firauni wengine, mweleze,mwanzoni kabisa, kwamba "mwenzio pamoja na kuwa tu wapenzi, mie njia moja sitosheki, napenda na mferejini kwenye matope.{SI NDIO UMEAMUA KUWA SHETANI MDOGO}, mweleze ili ujue kuwa mtakua mashetani wawili au la, kuliko ukaigiza kuridhika kumbe huridhiki. YAANI IWE MWANAMKE AU MWANAUME, UKIONA TU MWENZI WAKO ANAINGIZA TABIA HII MBAYA NA CHAFU ISIYOFAA KATIKA JAMII. NAKWAMBIA HATA KAMA IWE NI NDOA YA KANISA MOJA, TAKATIFU, KATOLIKI, LA MITUME, KADAI AMA TOA TALAKA MAPEMA KABISA. Nikwambie, akimaliza kukuharibu wewe ataharibu na mwingine, na mwingine, mwisho atalawiti na kuwafundishha watoto wenu. Mwisho tunazalisha vifo na upasuaji wa kizembe kabisa katika vyumba vya uzazi kwaajili ya kuukumbatia ushetani huu.

Ambizaneni mapema kuwa mnataka mahusiano au ndoa ya aina fulani. Ambizaneni mapema kuwa hiki nakipenda na hiki sikipendi. Zipo tabia unaweza kusema hii nitaiweza, ama hii nitaivumilia, ukiona tabia hii siiwezi basi toka haraka kwenye mahusiano hayo, usisubiri mpaka kuita watu wakuamulie.

Wanawake wengi sana ni wahanga katika jambo hili. Pale mwanaume anapomfata kwa mara ya kwanza, anakuja kwa sura nzuri kabisa, akiambiwa fanya hivi anafanya, fanya vile anafanya, mkishazoeana tu. unaanza kuuona uhalisia wa tabia husika ya mwenzi wako. Ndoa au mahusiano huwa machungu wakati huo. Nikwambie waziwazi kabisa, ikiwa utaona mabadiliko hayo ni hatari kwa usalama wako achana nayo.

Katika yote, la muhimu ni kupendana kweli, hivi sasa kumeibuka hata walaghai wa mapenzi wa kike. Tumezoea kushuhudia wanaume ndio wakiwalaghai wapenzi wao, lakini hivi sasa tunashuhudia hata walaghai wanawake, iwe wana pesa au hawana. Ni muhimu kujua kuwa binadamu wote wana moyo wa nyama, hivyo maumivu halisi huyasikia. TUSIVUNJANE MIOYO YA KUPENDA.

***NAKUTAKIA HERI YA CHRISTMASS NA MWAKA MPYA, ANDIKO HILI LIKATUONGOZE KATIKA MAHUSIANO KWA MWAKA HUU WOTE. AMINA.***

***ASANTE NA KARIBU SANA.***

**Tunasoma kutanua mbawa zetu, safari, burudani na kujifunza. Hivi ndivyo vitabu nilivyo visoma na kukamilisha kwa mwaka 2024—MARKUS MPANGALA 'MNGONI'**

**1. KIFO SIKU YA FUNGATE—*Karl Mick Binamu***

Mwanaume alienda kuoa. Akapewa mke, na ndoa ikafungwa. Lakini wakiwa kwenye fungate anapanga njama za kumuua mkewe mpya. Kwanini? Mwandishi anakupa majibu.

**2. OPERESHENI KASHMIR-*Richard Mwambe 'Amata Ric '***

Usaliti katika Jeshi letu, na vita vya Kashmir ni simulizi ya kijasusi ambapo mwandishi anaelezea namna hujuma zinavyofanywa na watu wa '*kikulacho*'. Utapata historia, visa, mikasa na hekaheka nyingi za wahusika wake.

**3. HATIMA YANGU FIRENIA-*Atnas Garaba na Anastasia Mbelwa***

Waandishi wapya, wameleta simulizi ya aina yake kuhusu Ufalme wa Firenia (Tanzania?) sijui. Ila Binti ananyimwa uhuru wa kuishi na kujichagulia. Siku alipopata mabinti wa uswazi basi Firenia kuliwaka moto.

**4. NDEGE TUNDUNI - Japhet Nyang'oro**

Ni riwaya ya kijasusi ambayo ni mwendelezo mzuri kutoka Mhanga wa Msumbiji. Visa na mikasa ni vingi.

**5. MAJARIBIO YA MAPINDUZI DHIDI YA NYERERE - *Dk. Kamal***

Rais Nyerere alipendwa sana, lakini pia akapata maadui waliotaka aondoke madarakani. Kitabu kinaelezea majaribio ya Mapinduzi yalivyokuwa.

**6. YALIYONIKUTA TANGA - *Mohammed Mohammed Hammie Rajab***

Moja ya simulizi zilizonifanya nigombane na rafiki yangu mmoja. Tulikuwa tunasoma kwa zamu. Kama unapenda visa na mikasa ya mapenzi ya Tanga basi humu mwandishi amechora taswira nzuri. Kama kijukuu cha *Wangoni* nimetamani kuweka makazi Tanga.

**7. JUHUDI NA CHANGAMOTO -Sheikh Issa Ponda**

Mwandishi ni miongoni mwa Watanzania wenye mvuto na ushawishi. Ni mtu ambaye alinichochea sana kuzijua harakati zake. Ndani utajifunza harakati, ukachero, Mageuzi na masuala nyeti ambayo Sheikh Ponda alikuwa akipigania kwa jamii.

**8. MVULANA HATARINI-Doris Mboma**

Je maisha ya watoto wa kiume yakoje sasa? Mzazi na mlezi hiki ni kitabu chenu mnunulie mwanao.

**9. MWANANGU MPENDWA - *Bupe Berrums***

Endapo una mtoto wa kiume, hakikisha unamnunulia kitabu hiki chenye wingi wa maelezo yenye mifano hai kuhusu malezi na elimu ya rika.

**10. KUISHI KATIKA MALENGO - Oliva Kilungeme**

Maisha yanahusu watu. Na hao watu wana nguvu na wanaweza kujeruhi maisha yako yote. Kitabu hiki kinawafaa watu wa rika zote katika kujijenga binafsi.

**11. UJASUSI NI NINI NA MAJASUSI WANAFANYA NINI-Evarist Chahali**

Ukitaka kujua Stadi za kazi za ujasusi basi hiki ni kitabu kizuri cha kufanyia rejea toka kwa Jasusi mstaafu.

**12. SAIKOLOJIA YA BIASHARA - Suleiman Kijogoo**

Wanasema Kila biashara ina tabia zake tofauti na tabia za mfanyabiashara. Mchango wa Kila upande unaweza kuua au kuimarisha biashara.

**13. KIMWEKO; SIRI ILIYOFICHWA-Kambi Mbwana**

Riwaya kuhusu mapenzi na biashara ya dawa za kulevya. Mwandishi ameonesha umahiri katika utafiti juu ya mbinu za uuzaji wa dawa hizo, pamoja na mapenzi yasiyoelezeka ya mrembo Tatiana bila kujua Wala kufanya 'profiling' kuhusu mpenzi wake huyo ni nani.

**14. TARISHI-Hassan Mambosasa**

Una risasi moja tu, na jukumu lako ni kujilinda. Ukipoteza hiyo, maana yake adui anakumaliza.

**15. MUUAJI WA MWAKA MPYA-Hussein Hussein Issa Tuwa**

Mkusanyiko wa hadithi fupi, ambapo msomaji amependelewa kwa kweli. Kama wasemavyo wahenga, kosa la mwisho lina madhara makubwa na muuaji wa mwaka mpya ana kisirani Kibaya kwani amegundua njemba lake ni hanithi.

**16. HISTORIA YA SINGIDA-Alfred Ringi Nyalandu**
Kitabu hiki kitakupatia simulizi za kihistoria za wakazi wa Mkoa wa Singida, ukoloni, Mila na Desturi, pamoja na vita vya Makabila mbalimbali. Nimependa simulizi za vita vya Wenyeji wa Singida na Wamasai.

**17. SARUFI KWA UJUMLA; UTUNGAJI NA UFAHAMU-Zakia Mbwana**
Kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili, kujiongezea uwezo na kinawafaa pia wanafunzi wa Sekondari na watu wazima.

**18. USIKU WA DENI-Gwamaka Mwamasage**
Riwaya ya kisiasa kuhusu masuala ya vita vya uchaguzi, mapenzi, uzazi na mazingira yake.

**19. NDOANO-Japhet Nyang'oro**
Riwaya ya kipelelezi ambayo inaangazia Misheni mbalimbali za vyombo vya Dola katika ulinzi na usalama.

**20. CHOOSE YOUR ENEMY WISELY; Business Planning for the Audacity Few - Patrick Bet-David**
Kwenye biashara, kazini, kampunini, kiwandani, Taasisi ama hapo kwenye Menejimenti tofautisha kati ya mshindani wako na adui yako. Biashara inaweza kuwa na adui, wewe unaweza kuwa na adui, lakini mshindani si adui yako. Chagua vema vita hivi; chagua vema marafiki na aina ya ushirikiano. Kinafaa kwa wafanyakazi, Wafanyabiashara, wamiliki wa Taasisi au kampuni.


**21. BUSINESS AS USUAL IN BLOODIED LAND?;- Role of Business in Forced Evictions In Loliondo, Tanzania (Amnesty International).**
Kinazungumzia masuala ya uhamishaji wa Wamasai kutoka maeneo yao kwenda kwingine.

**22. MY STORY - Mohammed bin Rashid Al Maktoum** Kama una ndoto za uongozi hiki ni kitabu kizuri sana.

**23. INVINCIBLE; Inside Arsenal's Unbeaten 2003-2004 Season - Amy Lawrence**
Kitabu kinahusu masuala ya uongozi katika Taasisi yako. Kinafaa kwa wale waliopo kwenye Menejimenti na wapenzi wa Soka.

**24. NIMEANDIKA MISWADA YA VITABU. UTAJUTA KUNISOMA MAANA KAMWE HUTOACHA.**

MARKUS MPANGALA
Anuanipepe; mawazoni15@gmail.com




**MARKUS MPANGALA 'Mngoni', Mwandishi, Mchambuzi, Mhariri wa miswada mbalimbali. Ukifika Morogoro, hakikisha unapita Stendi ya Daladala ya BIMA au SAMAKI SAMAKI ujinunulie vitabu kutoka dukani kwake.**



**HAPPY BIRTHDAY EMMANUEL KINDO**

Ngurumo ya Mwandishi tunakutakia kumbukizi njema ya siku yako ya kuzaliwa.

Mwenyezi Mungu akujalie mema mengi na akutimizie hitaji la moyo wako.

*Endelea kutufanyia magrafiks*

*Dec. 25

**KATIKA safu yetu ya MIAMBA WA AFRIKA, leo tunakuletea Patrice Lumumba. Huyu alikuwa Waziri Mkuu wa nchi ya Congo DRC. Ni mmoja kati ya waafrika wachache waliokataa kuwa vibaraka wa wakoloni, alipambana kuikomboa Kongo, lakini nini kilimkuta? Tuendelee...**



Patrice Lumumba

**SEHEMU YA 3**

Ganshof alirudi Kongo tarehe 12 Juni 1960. Siku iliyofuata, alimteua Lumumba kuhudumu kama mjumbe *(informateur)* aliyekuwa na jukumu la kuchunguza uwezekano wa kuunda serikali ya umoja wa kitaifa iliyojumuisha wanasiasa wa mitazamo mbalimbali, na kuweka tarehe ya mwisho kuwa 16 Juni 1960.

Siku hiyo hiyo ya uteuzi wa Lumumba, muungano wa upinzani wa bunge, *Cartel d'Union Nationale,* ulitangazwa. Ingawa Kasa-Vubu alikubaliana na mawazo yao, alijitenga nao. MNC-L pia ilikuwa na matatizo ya kupata uungwaji mkono wa PSA, CEREA *(Centre de Regroupement Africain),* na BALUBAKAT *(Association Générale des Baluba du Katanga).* Mwanzoni, Lumumba hakuweza kuwasiliana na wanachama wa cartel. Hatimaye, viongozi kadhaa waliteuliwa kukutana naye, lakini misimamo yao ilibaki imara. Tarehe 16 Juni 1960, Lumumba aliripoti matatizo yake kwa Ganshof, ambaye aliwapa muda na kuahidi kuwa mpatanishi kati ya kiongozi wa MNC-L na upinzani.

Baada ya Ganshof kuwasiliana na uongozi wa cartel, alishangazwa na ukaidi wao na uhakikisho wa msimamo mkali wa kupinga Lumumba. Kufikia jioni, juhudi za Lumumba zilionekana kuwa na nafasi ndogo za kufaulu. Ganshof alifikiria kumpa nafasi ya *informateur* Cyrille Adoula na Kasa-Vubu, lakini alikabiliwa na shinikizo kutoka kwa washauri wa Ubelgiji na Wakongo kumaliza jukumu la Lumumba.

Siku iliyofuata, tarehe 17 Juni 1960, Ganshof alitangaza kuwa Lumumba ameshindwa na kumaliza jukumu lake. Kwa kufuata ushauri wa Ganshof, Baudouin alimteua Kasa-Vubu kama formateur. Lumumba alijibu kwa kutishia kuunda serikali yake na kuiwasilisha kwa bunge bila idhini rasmi. Alifanya mkutano katika OK Bar huko Léopoldville, ambako alitangaza kuundwa kwa serikali ya "watu" kwa msaada wa Pierre Mulele wa PSA. Wakati huo huo, Kasa-Vubu, kama Lumumba, hakuweza kuwasiliana na wapinzani wake wa kisiasa.

Kasa-Vubu alidhani angepata urais, kwa hivyo alianza kutafuta mtu wa kuhudumu kama waziri mkuu. Wengi wa wagombea aliowazingatia walikuwa marafiki waliokuwa na msaada wa kigeni kama wake, wakiwemo Albert Kalonji, Joseph Iléo, Cyrille Adoula, na Justin Bomboko. Kasa-Vubu alichelewesha kufanya uamuzi wa mwisho.

Tarehe 18 Juni 1960, Kasa-Vubu alitangaza kuwa alikuwa amekamilisha serikali yake na vyama vyote isipokuwa MNC-L. Alasiri hiyo, Jason Sendwe, Antoine Gizenga, na Anicet Kashamura walitangaza mbele ya Lumumba kuwa vyama vyao havikuwa vimejitolea kwa serikali hiyo. Siku iliyofuata, tarehe 19 Juni 1960, Ganshof aliwaita Kasa-Vubu na Lumumba kwenye mkutano ili kufikia mwafaka. Hii ilishindikana baada ya Lumumba kukataa wazi nafasi ya waziri mkuu katika serikali ya Kasa-Vubu.

***Itaendelea toleo lijalo!***

# SAKO KWA BAKO:

## EMMANUEL MOSES KINDOLE

**Happy birthday kwa mtaalamu wetu wa ma-graphics… huyu ni nani?**

Jina langu halisi naitwa Emmanuel Moses Kindole. Nakumbuka wakati nipo shule ya msingi, darasani mwetu kulikuwa na wakina Emmanuel wengine kama wanne hivi, hivyo kufanya idadi yetu tuwe watano. Hii ikawa inaleta mkanganyiko baina yetu. Maana mwalimu au mwanafunzi mwenzetu alipoita jina la mmoja wetu tukajikuta wakina Emma' wote tumeitika kwa wakati mmoja. Wajina wangu walikuwa wanaifurahia sana ile hali, ila kwangu ilikuwa inaniudhi sana hata nikaondokea kujibadili jina *(siyo official)* na kuligeuza kuwa **Kindo Emmanuel,** hivyo nikadumu nalo hadi Leo.


Tangu nikiwa bwana mdogo nilikuwa napenda sana kusoma vitabu hasa vya simulizi, na ndoto yangu kubwa ilikuwa nije kuwa mwandishi ili maandishi yangu yawe maktaba, yaje yasomwe na vizazi hata vizazi. Hivyo nilijifunza fasihi kwa bidii. Mwaka 2009, wakati huo ndiyo mitandao ya kijamii inaibuka nikajiunga na mtandao wa *Facebook*. Pia wakati huo Simujanja zilikuwa chache sana nikawa naenda *Internet Café* (Pale Magomeni, Sea Boys, ilipokuwa ofisi ya Ras Simba) na kuanza kuandika na kupost simulizi zangu za; Msafiri, Taxi ya Kijivu, *My Strange Friend* (ya lugha Kiingereza), Mateka n.k. Ila, kwakuwa napost simulizi huku nikiambatanisha na jalada (ambalo niliDesign mwenyewe) hivyo waandishi wengine nao kumbe walikuwa wakinifuatilia. Baadaye wakaanza kujitokeza kwa wingi wakinipa niwaundie majalada kwa ajili ya kazi zao. Hivyo nikajikuta muda wangu mwingi *(wa ziada, ambao ningetakiwa kufanya kazi zangu binafsi za uandishi nikajikuta nautumia katika kuunda majalada ya kazi za waandishi),* nikajikuta sipati muda wa kuandika tena *seriously* kwa manufaa yangu binafsi, ila kwa upande mwingine si kwamba nilipoteza ndoto/azma yangu ya tangu udogoni, ya kuwa maktaba katika vitabu, hasha! Ilitimia. Kwasababu licha ya kwamba sikuchapa kitabu changu binafsi, lakini jina na chapa yangu imeendelea kuwepo maktaba katika vitabu vingi vya waandishi wa Sasa.

***Hebu tueleze, hii graphics, unaifanya tu kwa utundu au ulisomea shuleni?***

Mwanzoni kabisa nilikuwa nafanya *Fine Art* yaani uchoraji wa kawaida kwa kutumia kalamu, brashi na rangi za aina aina. Sasa mwaka 2006 nikiwa kidato cha 2, Kuna *brother* mmoja aligundua kipaji changu, yeye ni *Professional Graphic Designer* mpaka leo anaendelea...hivyo ananiambia kuwa nikijifunza *Graphic Desiging* nitakuja kuwa *'noma'* sana, maana dunia inaenda mbio sana, tunaingia kwenye teknolojia na uchoraji wa mikono hautakuwa na shughuli nyingi. Nikakubali wazo lake hivyo ikawa kila siku nikitoka shuleni siendi tena *tuition* pale Mchikichini (tunapaitaga Mchiki Down, Waliosoma shule za Dar' lile chimbo siyo geni kwao) Kwangu nilikuwa na wakati mgumu sana, Yaani nijifunze *Graphic Designing* na kujifunza kuitumia kompyuta kwa wakati mmoja....ila nilikaza. Naye alinifundisha kwa bidii na upendo kuanzia A mpaka Z, na nilipokuwa nimeiva akaniajiri kwenye ofisi yake ya *Printing* pale Kariakoo Hebu vuta picha, unaajiriwa na mwalimu wako!

Na katika hili pia kwa upande fulani ilinipa tena wakati mgumu, kwani ilinitaka nilinganishe mzani kati ya kazi na shule, maana wakati huo nimepata ajira nipo kidato cha tatu. Nikirudi katika swali husika ni kwamba baada ya kujifunza na kuielewa, siku za mbeleni nilienda Chuo kuisomea zaidi ili niwe na cheti kinachotambulika *(ingawa ningeweza kutengeneza cheti feki na vikafanana kabisa , yes! Maana vyote hutengenezwa na designers),* nikasoma na kozi nyinginezo za *Multimedia* kama *Videography and Photography*, *Music Producing* n.k

***Mahojiano haya yataendelea katika toleo lijalo…***



EMMANUEL MOSES KINDOLE "KINDO"

# SHAJARA YA MUUAJI—10

Na. Richard Mwambe



**Akamgusa begani yule ambaye kidogo alikuwa na unafuu na kazi. Yule kijana akasimama kwa ukakamavu na kutoa saluti, maana Ngai alikuwa juu kwa cheo.**

***Endelea...***

"Samahani afande, swali dogo... Najua we umekaa hapa Chang'ombe miaka mingi kidogo..." Akamwambia.

"Ndiyo afande!" Akajibu yule PC

"Unamfahamu Inspekta Damasi na Steven ?"

"Ndiyo afande!"

"Wako wapi kwa sasa?"

"Kila mmoja alipata uhamisho kwa muda wake... Damasi nafikiri alipelekwa Bunda na Steven alipelekwa Sumbawanga, zaidi ya hapo sijui kwakweli," yule askari akaeleza.

"OK, asante nitauliza ofisi..." Ngai Mathola akamshukuru yule kijana na kutoka pale akaelekea moja kwa moja kwa mkuu was kituo. Lililompeleka kule ni ruhusa tu. Ngai aliomba kuchelewa kufika kazini siku inayofuata akisingizia anafika kwanza hospitali. Hiyo ilikuwa janja yake tu. Tayari kichwani na kwenye kile kijitabu chake alisuka mpango wa siri wa kupita kwenye nyayo zote za kesi hiyo. Mkuu wa kituo hakuwa na tatizo, badala ya kukubali kuwa askari huyo achelewe kufika, alimwambia asije kabisa ili aangalie afya yake. Ngai akatoka mle ofisini akiwa na furaha sana.

Jioni ya siku hiyo ilimkuta mitaa ya Tandika. Akiwa kavaa juba lake pasi na kuogopa joto la jiji hilo. Hatua zake ndogondogo zikamfikisha kwenye kijiwe cha kahawa. Pale vijana kadhaa walikuwa wameketi na wazee wakijiburudisha.

"Asalaam aleikum!" Akawasalimu. Wale wanywa kahawa nao wakaitikia kwa pamoja huku macho yao yakiwa kwa mwanamke huyo.

"Samahani, naulizia gesti inaitwa Mibingiriko... Gesti ya zamani hivi...". Wale watu badala ya kujibu wakatazamana.

" Astakafulilah!" Mzee mmoja aliyekuwa na balaghashia akatamka. "Nenda hivi, mtaa wa kwanza wa pili ule wa tatu ingia kushoto ifuate hiyo njia mpaka kwenye kona hivi utaiona hapo kulia...!" Kijana mwingine akatoa maelekezo. Yule mzee akainua kichwa na kumwangalia mwanamke yule akiianza safari kuelekea huko, "mi nalijua ataulizia masjid... Aulizia gest... Jamani dunia inafanya kazi!" Akasema na wote wakaangua vicheko.

❦❦❦

Mibingiriko Guest House bado ilikuwa palepale, haikuhama. Tofauti tu ni kwamba sasa ilikuwa chakavu, haikuwa na utunzaji. Kama imetelekezwa vile. Ukimya uliitawala, mlango wa mbele ilikuwa umefungwa lakini kibao kilichoonesha 'vyumba vipo' kilikuwepo hapo maandishi yake yalisomeka kwa taabu.

Akaujongelea ule mlango na kugonga. Ngai akapokelewa na mwanadada aliyeonekana kuwa mtu mzima kidogo. Mwanamke huyo alikuwa wa kawaida tu, yule wa uswahilini.

"Karibu Dada!" Akakaribishwa. Yule mwanamke alimwangalia Ngai, aliwajua wateja wake wa kila siku. Siku hizi Mibingiriko haikuwa tena ya kulaza wageni bali, ilikuwa ya *short time*.

"Asante... Samahani, namuulizia Dada mmoja anaitwa Ujoro, sijui nitampata maana nimeona nianzie hapa..." Ngai akamwambia yule mwanamke.

"Ujoro ndiye mimi!"

"Oh nashukuru... Sijui tunaweza kukaa mahali tukaongea?"

"Karibu ndani..."

Ngai akaingia na kuketi kwenye kochi kuukuu lililompokea na kelele za mbao zilizochoka. Akafikiri atadondoka kwa jinsi alivyoshituka.

"Pole hauanguki!" Ujoro akamwambia. "Ndiyo Dada karibu nakusikiliza, mi ndiyo Ujoro..."

"Sawa Ujoro... Mi naitwa Hafsa, nyumbani kwetu ni kule Chang'ombe Mchicha..."

"Ndiyo!"

"Japo kwa muda mrefu sana nimeishi Mascut... Ni Mdogo wa mwisho wa marehemu Aziza!" Alipojitambulisha hivyo, Ujoro akaonekana kushika kifua chake yaani moyo kama umeruka hivi. "Unamkubuka?"

"Namkumbuka sana shoga wangu Aziza, Alifia chumba kileee" akaonesha kwa mkono. "Sasa ulitaka msaada gani tena kwangu?"

"Ujoro, Dada yangu keshakufa... Lakini Nina wasiwasi kuwa hata wale waliofungwa kwa ajili ya hicho kifo wakawa si watu sahihi..." Ngai akaeleza.

"Usiseme watu, ni mtu... Niseme ukweli, mimi nilipanda kizimbani kama shahidi, ushahidi wangu umemfunga kijana mmoja muuza maji anaitwa Magena Makange... Alikuwa mpenzi wa Az-

# SHAJARA YA MUUAJI—10

iza kwa siri sana lakini walipendana.... Usinikumbushe nyakati zile!" Ujoro akaeleza. Ngai akakaa vizuri kusikiliza maelezo hayo. Huku kinasa sauti chake ndani ya lile juba kikiendelea kufanya kazi.

"Makange Magena! Unasema alikuwa muuza maji...?"

"Ndiyo ni kijana alikuwa anatembeza maji, yaani hata ungemuona, husingeamini kama anatoka na Aziza..."

"Sisi wanawake tuna mambo mengi Ujoro... Unaweza kuwa na mume au bwana anayekupenda kwa dhati, anakupa kila tu lakini ukatembea na muuza madafu... Umaana wa mwanamke katika maisha siyo pesa wala nini ni kile kinachomfurahisha akikipata, basi!" Ngai akaeleza. "Sasa Ujoro, mi napenda kujua kitu kimoja siku dada angu alipouawa nani na nani unaowakubuka walikuwa eneo hili LA gesti?"

Ujoro akatulia kwa jozi la sekunde, akawaza na kuwazua, kichwa chake kikawa kinarudisha kumbukumbu nyuma.

"Nilikuwa Mimi kama mfanyakazi, Aziza mwenyewe, Mgeni wake Bwana Merengo, akaja na huyo Magena... Halafu vyumba vitatu vilikuwa na watu siwakumbuki majina maana walikuwa wa kupita tu..."

"Zaidi ya wewe au hao wengine hakukuwa na wafanyakazi usiku huo?" Ngai akauliza.

"Mfanyakazi kwa usiku nilikuwa mimi labda na mlinzi..." Ujoro akajibu.

"Mlinzi anaitwa nani?"

"Mzee Hamisi Makisu au mwite Mikogo... Sijui yuko wapi yule mzee si ajabu ameshakufa..." Ujoro akajibu. Ngai akabaki kimya akitafakari huku macho yake yakiwa yanatalii kuta chafu, nyeusi za gesti hiyo.

"Naweza kuona chumba alichofia? Au kina wageni?" Akauliza.

"Hapana, leo sijapokea mgeni, njoo..." Ujoro akamwita Ngai na kumwongoza mpaka kwenye kile chumba.

Akaingia na kukitazama vizuri. Sakafu, kuta, kitanda cha kizamani, madirisha yaliyotoboka nyavu na vyoo vyake vilivyovunjika. Juu akatazama dari safi ya TNT iliyotengenezwa kwa mkono makini. Kwenye lile dari palikuwa na mlango wa kuweza kupandia juu kama kuna hitajika matengenezo. Aliporizika na Yale aliyoyaona, wakarudi pale walipoketi na kujimwaga tena.

Tsh 4000/= Softcopy. Lipia Mpesa Lipa Namba 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Whatsapp 0766974865

"Wangapi mlilala selo?"

"Mimi na wageni waliokuwepo usiku huo, lakini baada ya upelelezi wakaachiwa, hawakuonekana kujua kitu. Mimi tu niliachwa kwa dhamana lakini ilibidi nitoe ushahidi mahakamani..." Ujoro akaeleza.

"Mlinzi hakuhojiwa?" Ngai akauliza.

"Mh! Sikumbuki, ila tulipoondoka hapa kupelekwa polisi yeye hakuwa mmoja wetu, nafikiri hakuhojiwa..." Ujoro akaeleza.

"Labda ye kwakuwa ni mlinzi angeweza kujua jambo... Unajua anapoishi?"

"Hapana, na hata sijamwona miaka mingi sasa..." Ujoro akaeleza.

"Nashukuru sana Ujoro... Mi nafuatilia tu nijue, nilikuwa nampenda sana dada yangu!" Ngai akamwambia Ujoro kisha wakaagana. Akampa na bakshishi ya shilingi elfu tano. Ujoro akashukuru na kufurahi sana. Wakaagana. WP Ngai Mathola akaondoka eneo lile.

Kwa siku hiyo ilitosha yale aliyoyasikia na kuona. Sasa ilikuwa wakati wa kuweka taarifa hiyo vizuri kabla kukusanya taarifa nyingine. Mpaka hapo aliona keshapiga haua kubwa ya kuanzia. Ngai Mathola, Mkaguzi Msaidizi wa polisi, kituo cha Chang'ombe alianza kazi hiyo kwa siri. Huu ndiyo ilikuwa ulemavu wake, kufukua makaburi.

Akaitazama saa yake, bado ilikuwa inamruhusu kufanya zaidi. Akiwa kwenye daladala la kuelekea Kariakoo, hakushuka Keko ambako ndiko alikuwa akiishi akapitiliza mpaka Kariakoo. Huko akaelekea Feri, akavuka mpaka Kigamboni, Mjimwema. Nako aliulizauliza mpaka akampata nyuma ya Bwana Mathias Marengo. Tayari giza liliivamia nchi.

TAARIFA:- Riwaya hii ya Shajara ya Muuaji inakomea hapa. Kama wataka kuendelea kuisoma, waweza wasiliana na mwandishi kwa whatsapp 0766974865.
Toleo lijalo tutaanza riwaya mpya!

**Haikuwa shida, akaruhusu lile gari la vijana wa kazi kufuatana na Amata kwenda Kawe.**
**Usiku huohuo Amata aliwasili na askari wale mbele ya jumba hilo ambalo kwalo Marietha alihifadhiwa.**


***Endelea...***

Yule mwanamke kibonge alikuwa juu ya kochi akimsubiri Carlos, lakini mpaka muda huo bado alikuwa hajatokea. Michakacho ya miguu nje ya nyumba hiyo vilimfanya mwanamke huyo kukurupuka na kuuendea mlango pasi na kujua nani. Alipoufungua mlango, hamad! Akakutana na watu wanne.

"Polisi! Upo chini ya ulinzi!" Amata akamwamuru. Yule mwanamke akajikuta hana ujanja. Alitulia kama maji yatuliavyo mtungini, huku macho yakiwa yamemtoka pima. Jicho la Amata lilipotua kwake, halikupata muda mrefu kumtambua. Ni yeye! Akakiri kichwani mwake maana hata nguo bado alikuwa hajabadili. Jasmine akamtia pingu mwanadada huyo na kumkalisha chini.
"Kagua vyumba vyote," Amata akatoa amri huku yeye akizunguka huku na kule katika sebule hiyo, akikagua hiki na kile. Katika moja ya picha zilizokuwa katika sebule hiyo ambayo ilimvutia ilikuwa ni ya Carlos na Wazungu wawili, mmoja upande huu na mwingine upande wa pili. Akainyakuwa na kusogea nayo kwa yule mwanamke.
"Hawa ni nani?" Amata akauliza.
"Siwajui," akajibu kijeuri.
"Afande!" mmoja wa wale askari akaita.
"Sema!"
"Hatujaona kitu!" akasema.
"Hawa wamemteka msichana anaitwa Marietha, wamemficha humu ndani…"
"Marietha yuko wapi?" Jasmine akamuuliza. Yule mwanamke hakujibu. Jasmin akachomoa kisu cha kukunja na kukifyatua, "usiponambia, nakuchana ngozi yako bila huruma," akamwambia. Lakini bado hakuonesha ushirikiano. Jasmine alimkamata mkono yule mwanamke na bila huruma akachoma kisu kwenye nyama ya mkono.
"Aaaaaah! Yuko chooni!" akapiga kelele.

"Choo gani?" akauliza.
"Aaaaa usiniumize tafadhali… nasema dadaaa..!
"Haya sema!"
"Cha nje cha nje…" akajibu.
Wale askari haraka wakakimbilia nje ya nyumba hiyo na kuvunja mlango wa choo. Na kumkuta msichana yule akiwa kajilaza chini, katika sakafu chafu iliyokosa usafi kwa muda mrefu.
"Shit kuna watu makatili sana," askari mmoja alisema huku akiiweka bunduki mgongoni mwake. Wakati huohuo Jasmine alifika na kuingia ndani ya kile choo. Kabla ya yote alimpiga picha Marietha katika hali ile, kisha akamfungua zile kamba na kumwondoa yale matambaa kinywani mwake. Kamanda Amata akatoka nje na kukutana na hali hiyo. Macho yakagongana na msichana huyo aliyekosa nguvu kwa kipigo alichokipata usiku huo. Hakuongea neno, walimchukua na kuondoka naye. Yule mwanamke kibonge naye akachukuliwa na wote wakafikishwa Polisi Oysterbay. Saa tisa usiku Scoba aliwasili na kuwachukuwa wote wawili kisha wakaelekea pasipojulikana.

❦




Katika chumba cha mahojiano Carlos aliketishwa mbele ya Amata na Scoba, akiwa hana nguo na tayari alikwishapekuliwa katika kila kona ya mwili wake. Katika chumba cha pili Chiba, Gina pamoja na Madam S walikuwapo.
"Nataka unambie katika ile bahasha kulikuwa na nini?" Amata akauakauliza huku akiweka vizuri chano kilichojaa vifaa vya utesaji kama mikasi, praizi, bisibisi, keekee, vizu vidogodogo.

"We si ndiyo uliichukua na umeisoma, kwani hukuona nini kimeandikwa?" akajibu kijeuri.
"Simaanishi hilo, nataka unambie juu ya ile bahasha, ulikuwa unaipeleka wapi, na kilichoandikwa mle kilimaanisha nini?" akaongeza swali. Carlos hakujibu neno, alitulia kimya huku akiangalia kwa jicho la dharau. Amata akavuta hatua moja mbele na kukaa juu ya meza huku akimwangalia kijana huyo.
"Napenda sana watu manunda kama wewe," akamwambia kisha akachukua kitu kama mkasi na kusimama wima sakafuni.

# RIWAYA: CRONOC 7 (19)- richard MWAMBE

"Sasa unataka kunifanya nini wewe?" akalalama Carlos.
"Naanza na sikio hili… kisha hilo… kisha nakupasua korodani… kisha nakuvunja miguu… baadae nakukata kidole kimoja baada ya kingine. Kufa hutokufa ila cha moto utakiona," akamwambia na kumkamata kichwa chake kwa nguvu. Kile kifaa kama mkasi kikakamata nyama ya sikio na akaanza kukibana taratibu huku makali yake yakikata sikio.

"Aaaaaaah ahhhhhh! Nasema niachee!" akapiga kelele za uchungu.
"Ukisema ndiyo nitakuacha!" Amata naye akapiga kelele huku bado akiendelea kukata lile sikio polepole na damu zikimmwagikia kijana huyo mabegani.
"Agenda, Agenda, agenda za mkutano, aaaaaaaiiigh!" akajibu huku akilia.
"Mkutano gani? Ulifanyika wapi?" akamuuliza huku akiendelea kukata lile sikio.
"Aaaaa wewee unaniumiza aaaahhhh! Mkutano wa wakuu, ulifanyika Nairobi…"
"Nairobi eee?..."
"Ndiyo!"
"Lini?"
"Niache basi nikuelezeeeee mamaaaaa unaniumiza! We jamaa shetani kabisa!" akalia kwa uchungu huku akijitikisa lakini kichwa chake hakikuweza kutoka kwenye kono lenye nguvu la  Kamanda Amata.

"Umeliona sikio lako hili?" akamwonesha kipande cha sikio alichokikata kikiwa kinaning'inia kwenye kile kimkasi, "haya sasa nieleze, ukikaidi naondoa na hilo lingine," akamwambia na kukitupa kando kile kipande.
"Aseee aaaaa ….!" Akaendelea kuuguza maumivu.
"Semaaaa sasa!" Amata aling'aka na kuinua bastola, akavuta slider na kuiweka tayari kisha kidole chake kikavuta nyuma kifyatulio, risasi moja ikafyatuka na kupunyua sikio lililobaki, na ule ukelele ulifanya kila mtu kuinama chini. Carlos alijikuta mkojo umemwagika pasi na yeye kujua. Mwili ulitokwa jasho la dharula akatetemeka kama mgonjwa anayehisi baridi kali.
"Utasema au husemi?" akamwuliza.
"We-we-we… ni-ni-niue tu!" akajibu kijeuri.

Amata akamwekea mtutu juu ya paja, "navunja mguu! Nivunje?" akamwuliza lakini jamaa hakujibu neno. Akarudisha basbastola na kuchukua kile kimkasi tena akamzunguka na kushika kichwa kwa kono lingine, akaweka ule mkasi katika sikio akalibana barabara na kuanza kulikata vilevile kama lile la mwanzo.
"Niacheeeee nakueleza…"
"Eleza…"
"Aaaaahhh ulifanyika siku nane zilizopita aaaaaiiiii, naumia bwanaaaa ms*nge wewee," akajibu huku akilia na kupiga makelele.
"Haya Cronoc 7 maana yake nini?" akamtupia swali.
"Hiyo sijui, kweli vileeeee… aaaaa, ila walikutana kuzungumzia hiyooo mamaaaa we!" akaendelea kulia. Amata akamwonesha kipande cha sikio la pili.

"Sasa hauna masikio, kinachofuata ni kukupasua korodani," akachukua kifaa kingine kinachofanana na kijiko kwa mbele lakini kiliunganishwa katikati kama koleo, akakizungushazungusha. Amata akaihukua ile tiketi ya ndege kutpka mfukoni mwake, akamwonesha.
"Na hii tiketi je? Unaishi Nairobi au Dar es salaam?" akamuuliza.
Carlos akabaki katumbua macho. Alishangazwa na weledi wa kijana huyo jinsi alivyokusanya yote hayo na kwa muda mfupi.
"Haya, nambie kwa hapa Tanzania washirika wenu wako wapi?" akauliza.
"Wengi tu, wengi sana hata mkuu wako wa nchi ni mshirika wetu…"
"What?"
"Unashangaa nini we si umetaka kujua?" Carlos akaongea huku akionekana wazi bado ana maumivu makali ya kukatwa masikio yake.

"Ok, *good!* Sasa kwa nini ile bahasha ilikuwa Baraza la Maaskofu?" nambie.
Wakati Amata anauliza swali hilo Carlos akajiinamia, akawa kama mtu mwenye kwikwi au anayeshindwa kumeza kitu fulani.
"Anajiua huyo!" Scoba alipiga kelele akatoka haraka pale alipo. Akambana kaakaa lake na kujaribu kumfanya ateme kile alichokuwa anakimeza. Carlos akamng'ata vidole kwa nguvu zake zote.
"Aaaaaaaiiiigggghh! Shiiiit!" Scoba akapiga kelele, kisha akamtwanga kichwa cha maana na Carlos akaachia ule mkono.

Lakini tayari alikuwa amefanikiwa kukimeza kidoge kile kidogo, povu likaanza kumtoka kinywani. Amata akatikisa kichwa kwa masikitiko, mlango ukafunguliwa Madam S akaingia.
"Vipi?" akauliza.

***Itaendelea...***

***Endelea...***
Akafungua mfuniko wa ule mtungi wenye mafuta na Alibaba akachungulia ndani yake. Kisha akanyanyua macho kumtazama kiongozi na kutabasamu.

"Karibu sana ndani ukae," alisema Alibaba. " Walete punda wako uwani huku."

"Ahsante sana. Una roho nzuri sana," alisema kiongozi wa wezi. Kisha akawaongoza punda wale mpaka ndani.

"Naona pia punda hawa wanahitaji chakula na kupumzika," Alibaba alimwambia kiongozi wa wezi. "Watue hiyo mizigo yao chini na wapeleke kwenye zizi. Wape nyasi huko na maji ya kutosha."

Hivyo kiongozi wa wezi akashusha ile mitungi na kuwapeleka punda kwenye zizi. Akaiacha ile mitungi arobaini kwenye uwanja wa ndani wa nyumba ikiwa imepangika kwa mstari mmoja.

"Unaweza tu ukaiacha mitungi hii hapo uwanjani haina neno kwa usiku mmoja," alisema Alibaba. "Twende ndani nikakupatie chochote ule ili upumzike."

Akamkaribisha yule kiongozi wa wezi ndani na kumuita Marjane mtumishi wake.

"Mke wangu yuko wapi?" Alibaba alimuuliza Marjane.

"Wameenda kulala. Wote na mwanao pia leo wameingia ndani kulala mapema sana." Alijibu Marjane.

"Sawa basi, Marjane. Mtengenezee chakula huyu mtu, tafadhali." Alisema Alibaba. "Ni mgeni wetu na ni vema tukamkirimu."

Marjane akavuta pumzi za kuonekana kuchoka. Alikuwa ameshachoka na kazi za siku ile na alikuwa anajiandaa kwenda kulala.

"Sawa bosi," Alijibu Marjane na kuelekea jikoni. Muda mfupi tu chakula kilikuwa tayari.

Kiongozi wa wezi alikula vizuri sana usiku ule, Marjane alimuandalia wali wa njegere na nyama na alifaidi sana chakula kile.

"Mpango wangu unaenda vizuri sana." Alijisemea moyoni. "Muda si mrefu Alibaba atakuwa mtuhumiwa wangu."

Alibaba akaingia jikoni wakati Marjane akiosha vyombo vilivyotumika usiku ule.

"Naenda kulala sasa," alimwambia. "Marjane, tafadhali hakikisha mgeni wetu anapata kila kinachohitajika. Asubuhi nitenda mapema sana kuoga hivyo nitahitaji sabuni na taulo."

Hivyo Marjane akaenda kumchukulia sabuni na taulo na Alibaba akaenda kulala. Kiongozi wa wezi akamwambia Marjane kwamba angependakupata hewa safi ya nje kidogo kabla ya kwenda kulala.

Kiongozi wa wezi akatoka nje mpaka uwani. Akasimama mlangoni kwa muda kidogo na akavuta pumzi, kisha kwa taratibu akaanza kuangalia huku na huku ili kuhakikisha kwamba hakuna mtu yeyote anayemtizama. Mbele yake ilikuwa ni ile safu ya mitungi yake aliyokuja nayo ambayo mifuniko yake ilikuwa iko wazi kidogo na ndani yake kuna wezi na walikuwa wamekaa kimya sana.

Akasogea karibu na mtungi wa kwanza, akainama kidogo kisha akaugonga pembeni kwa ishara ya kumuita aliye ndani yake, kisha akafungua mfuniko na kumnong'oneza mwizi wa kwanza kwenye ule mtungi.

"Sikiliza kwa makini!" alimwambia. "Hii ni sehemu inayofuata ya mpango wangu. Ukifika muda wa mashambulizi, nitarusha vijiwe kutoka katika dirisha la chumba nitakacholala. Vitaangukia huku uwani, mkivisikia tu tokeni na panga zenu na mkiwa tayari kushambulia. Nitakuja na mimi kuungana na nyinyi na kisha mwishowe tutamuua huyu Alibaba mwizi wa mali zetu!!"

Yule kiongozi wao aliend kwenye kila mtungi na kuugonga pembeni ili kumuita aliye ndani yake na kumwambia maneno yale yale kama aliyomwambia mwizi aliye kwenye mtungi wa kwanza. Kisha katabasamu na kupangusa mikono yake. Mpango ulikua unaenda vizuri sana.

**Je unahitaji kitabu chenye simulizi hii ya ALIBABA NA WEZI 40? Wasiliana nasi kwa WhatsApp 0766974865**



# BRITTLE PAPER YAITAJA MKUKI NA NYOTA KUWA NI 'PUBLISHER' BORA WA 2024

MKUKI NA NYOTA si jina geni miongoni mwa wapenzi wa vitabu nchini na hata nje ya nchi. Tunaweza kusema kuwa ni 'Mwamba' katika uga wa uchapaji na uchapishaji wa vitabu nchini. Lakini si hilo tu bali pia ni mdau mkubwa sana wa elimu hapa nchini na juhudi zao zinaonekana wazi katika kulisukuma gurudumu la elimu.

Hawa ndiyo wachapishaji wa vitabu mbalimbali vya ziada na kiada na pia hata vile vya wasifu na tawasifu za viongozi wakubwa na mashuhuri hapa nchini na zaidi ya hapo.

Brittle Paper limeandika: Tunayo furaha kutaja Mchapishaji Bora wa Brittle Paper Mwaka 2024 kuwa ni Mkuki na Nyota . Jumba hilo la uchapishaji lenye makao yake makuu nchini Tanzania lilianzishwa na Walter Bgoya ambaye pia aliwahi kuwa mhariri mkuu hadi alipokabidhi madaraka kwa mtoto wake Mkuki Bgoya baada ya kustaafu hivi karibuni. Kwa tuzo hii, tunasherehekea kujitolea kwa Mkuki na Nyota kutengeneza nafasi kwa fasihi ya lugha ya Kiafrika kustawi.

Mkuki na Nyota inafafanua upya maana ya kuweka kati lugha za Kiafrika katika uchapishaji. Wakati ambapo lugha nyingi za kiasili zinatatizika kushindana katika nyanja ya vyombo vya habari vya kimataifa vinavyotawaliwa na Kiingereza, Mkuki na Nyota amejitolea kimakusudi katika fasihi ya Kiswahili.

Katika muongo mmoja uliopita, wametoa takribani machapisho 30-40 kila mwaka, na katika mwaka mmoja ilivunja rekodi kwa kuchapishwa kwa vitabu 60. Katalogi yao inajumuisha maandiko bunifu, yasiyo bunifu na fasihi ya watoto.

**Walter Bgoya ni nan?**

Bgoya alizaliwa Ngara, Mkoani Kagera, mwaka 1942. Alikulia katika jamii ya kimwinyi chini ya ukoloni wa Waingereza, iliyozungukwa na utata wa kitabaka na madaraka. Wazazi wake, ingawa walikuwa na asili ya wakulima, walimiliki ardhi kubwa, huku mama yake akisimamia mashamba.

Baba yake, mmoja wa wanaume wachache waliosoma katika eneo hilo, alifanya kazi kama mwalimu wa kilimo na aliweka mfano wa uwajibikaji na uongozi.




Mnamo 1961, Bgoya aliondoka kwenda Amerika kwa masomo ya chuo kikuu, huko alikumbana na ubaguzi wa rangi chuoni na kujihusisha na harakati za haki za raia. Miaka hii iliimarisha mwamko wake wa kisiasa na kuchochea kujitolea kwake kenye masuala ya haki. Aliporejea Tanzania, alijiunga na Wizara ya Mambo ya Nje na alitumia miaka saba kuunga mkono harakati za ukombozi wa Afrika kupitia Kamati ya Ukombozi ya OAU. Alifanya kazi kwa karibu na wapigania uhuru Kusini mwa Afrika na aliunga mkono harakati za kupinga ubeberu kote ulimwenguni.

*"Nilitaka kuchapisha vitabu vilivyofichua kuwepo kwa miundo ya unyonyaji ya kikoloni na ukoloni mamboleo ambayo ilifanya uhuru wa nchi zetu kuwa wa udanganyifu. Wasomi wa Kiafrika wana jukumu la kuhamasisha umaskini wa siasa katika nchi zetu zinazoendana na masilahi ya nje kwa hasara ya watu wetu. Nilijitolea kwa nguvu zangu kwa kazi hii, sio tu ndani, na kwa nchi yangu bali pia kwa ulimwengu mpana wa Afrika.*

Alianzisha Mkuki na Nyota kwa sababu alitambua kuwa vitabu vinaweza kufungua akili na pia kukabiliana na pengo lililokuwepo katika uchapishaji wa fasihi ya kimaendeleo inayozalishwa nchini katika tanzu za kitaaluma na tanzu nyinginezo, hasa zile za waandishi wachanga wanaofanya kazi za tamthiliya, ushairi na sanaa. ***RM***

**Kutoka mtandaoni tumepata hivi vidokezo 35 vya kujisomea vitabu. Ungana na msomaji huyu aliyesoma vitabu 350 ili kujifunza zaidi.**

**Vidokezo 35 vya Kusoma Nilivyojifunza Baada ya Kusoma Vitabu 350+:**

1. Sehemu ngumu zaidi ya kusoma ni kukaa chini kuanza.
2. Acha kusoma vitabu vya kuchosha ili kutoa nafasi kwa vile vya kuvutia.
3. Kusoma kitabu kimoja kunaweza kusibadilishe maisha yako, lakini kusoma kila siku kutabadilisha kila kitu.
4. Soma vitabu vichache vilivyokuwa maarufu kwa siku, na zaidi vile vilivyodumu kwa miongo kadhaa.
5. Ukisema huna muda wa kusoma, angalia muda unaotumia kwenye simu yako.
6. Kusoma ni kusoma—jaribu vitabu vya kuchapishwa, *ebooks*, na vitabu vya sauti kupata aina inayokufaa.
7. Haijalishi unamaliza vitabu vingapi, bali ni vitabu vingapi vinakufikia kiundani.
8. Weka simu yako kimya na uiache chumbani kabla ya kusoma; utaongeza umakini wako mara 10.
9. Soma vitabu vizuri, soma tena vile vya kipekee, nunua upya vile vya kubadilisha maisha.
10. Huwezi kuwa msomaji kabla ya kuanza kusoma vitabu. Anza kusoma vitabu, ndipo utakuwa msomaji.
11. Ni bora kuacha kitabu kuliko kuacha kusoma kabisa.
12. Ukikutana na kitabu kilichokubadilisha maisha, jaribu kukisoma kila mwaka mara moja.
13. Rudisha, toa zawadi, au tumia tena vitabu usivyovipenda.
14. Kusoma kwa haraka ni kama kusoma mara mbili kwa haraka na kukumbuka nusu tu.
15. Sehemu bora za kusoma ni kwenye ndege, ufukweni, na bustanini.
16. Kipindi muhimu kwa kila msomaji ni kujifunza kuchagua vitabu mwenyewe badala ya kungoja kuchaguliwa na wengine (kama wazazi, walimu, au maprofesa).
17. Kusoma muhtasari wa vitabu na kufikiri umeelewa kitabu ni sawa na kutazama trela ya filamu na kufikiri umeelewa filamu.
18. Vitabu bora haviwezi kusomwa kwa haraka, kwa sababu hukulazimisha kusimama na kufikiri mara kwa mara.
19. Lengo la kusoma ni matumizi, si kukariri. Acha kutumia muda kukumbuka, badala yake tumia muda kutekeleza ulichosoma.
20. Ukiwa na lengo la kuanzisha tabia ya kusoma, anza kwa kusoma kwa dakika 2 kila siku.
21. Anayefaidika zaidi na muhtasari wa kitabu ni yule aliyeandika, si anayesoma.
22. Kama kitabu hakijabadilisha mawazo au tabia yako, basi kitabu hicho hakikufaa au hujajifunza chochote.
23. Kununua kitabu hakumaanishi umefungwa na mkataba wa kukimaliza.
24. Wanaosoma vitabu 100+ kwa mwaka mara nyingi wanalipwa kusoma au wanasoma hadithi za kubuni.
25. Hakuna mtu anayesoma kitabu kilekile mara mbili, kwa sababu kitabu hakijabadilika lakini mtu amebadilika.
26. Vitabu ni uwekezaji, si gharama. Kitabu cha $10 kinaweza kukuongezea $100,000 au hata $100 bilioni.
27. Mazingira ya kusoma ni muhimu zaidi kuliko motisha ya kusoma. Ni rahisi kusoma kitabu cha kawaida maktaba kuliko kitabu bora kwenye tamasha.
28. Beba kitabu kila mahali uendapo. Huwezi kujua lini utapata muda wa ziada wa kusoma.
29. Kipatie kitabu nafasi tatu (sura tatu) kukuvutia. Kama hakijakuvutia, acha na usijisikie hatia.
30. Njia rahisi ya kusoma: Pakua *ebook* au *audiobook* kwenye simu yako ili uwe na kitu cha kusoma kila wakati.
31. Sifa kubwa kwa mwandishi ni kuonyesha kwamba ulisoma, kuandika, na kupigia mistari kitabu chake. Kitabu safi kitamfanya afikiri hukukisoma.
32. Tumia muda zaidi kusoma vitabu vifupi. Baadhi ya vitabu vifupi vina mafunzo mazito zaidi.
33. Kwa matatizo ya daima, soma vitabu vya daima. Kwa matatizo ya kisasa, soma vitabu vya kisasa.
34. Vitabu ni mbinu bora zaidi za maisha: Kwa $10 unaweza kupata hekima ya miaka 10 kwa masaa 10 au chini.
35. Wakati bora wa kuanza kusoma vitabu ulikuwa miaka 10 iliyopita. Wakati wa pili bora ni leo.

Kutoka *Alex and Books*

Utaongeza vidokezo gani? Tutmie kwa Whatsapp **0766974865**

# KITABU NILICHOSOMA

## The Power of Discipline & From Mopping Floor…



**Juliana Isondo, Mwalimu 'Msomi' na mdau wa vitabu anatushirikisha kile alichojifunza kutoka katika vitabu hivi…**


Mwandishi anasema nidhamu binafsi (self discipline) inahitajika katika kila idara ya maisha yetu ya kila siku. Sambamba na hili nimejifunza yafuatayo

Hasara za kukosa nidhamu, mojawapo anasema mtu anapokosa nidhamu ni ngumu sana kutimiza malengo yake.


2. Watu wengi hawapendi mabadiliko kwasababu ya uoga wa kuchekwa hasa pale watakaposhindwa kutimiza malengo.

3. Watu wote waliofanikiwa katika maisha walifeli kwanza. Kufeli ni sehemu ya maisha.

4. Nidhamu na mpangilio ni vitu viwili visivyotenganishwa. Anamaana kuwa ili uweze kufanikisha malengo yako ni lazma uwe na mpangilio mzuri wa mambo na vitu vyako.




Watu wengi hawapo tayari kulipa gharama za mabadiliko. Unapoamua kubadili tabia fulani ambayo hupendezwi nayo usiogope maneno ya watu, marafiki na hata ndugu.
Kitabu ni kizuri saaana.
Hapo sijakimaliza ila kinavutia




5. kukisoma.

Kutana na Mwanamke aliyepitia magumu katika usichana wake. Alibeba mimba akiwa binti mdogo. Kabla ya miaka 25 alikuwa tayari na watoto watatu.
Yeye ndiye kichwa cha familia, anayetegemewa na watoto wake.

Akaamua kuacha kazi ya kuajiriwa akiwa mjamzito na kufanya jambo alilolipenda na lililobadilisha mustakabali mzima wa maisha yake. Pamoja na maisha yenye milima na mabonde amefanikiwa kutengeneza pesa ndefu. (Yeye anaita six figures per year!)
Nimejifunza vingi vichache vyake;

Kujenga mahusiano ni muhimu zaidi kuliko kuuza bidhaa.

2. Kitu cha kwanza katika biashara ni upendo na huduma. Ukiuza kwa upendo utauza zaidi.

3. Ukifanikiwa kutengeneza pesa nyingi usipandishe gharama za maisha yako. Live below your means.

4. Nyuma ya  mafanikio ya watu kuna vipindi vigumu ambavyo mfanyabiashara hupitia na maranyingi huwa havisemwi.

5. Mwenye kiu ya mafanikio anapaswa kuwa mwanafunzi wa kudumu.

Tujifunze, hii ndiyo maana nzima ya Kitabu Maisha



Richard Mabala, mwandishi wa kitabu Mabala The Farmer akimkabidhi kitabu Muasisi wa Anna Mbise Mobile Library Bi. Anna Mbise kama ishara ya kuunga mkono juhudi za mwanadada huyo ya uhamasishaji wa usomaji wa vitabu nchini.



Magwiji wa sanaa ya uandishi nchini, Bi Naheeda Ismail, Richard Mabala, Prof. Shivji, Omar Baajun na ... katika picha ya pamoja.



Muasisi wa Anna Mbise Mobile Library na Mwenyekiti wa UWAVITA katika picha ya pamoja na wadau wa usomaji wa vitabu aliokutana nao mapema mwezi wa Disemba.



HAPPY BIRTHDAY
IBRAHIM MARIJANI
GAMA

Ngurumo ya Mwandishi twakutakia kumbukizi njema ya siku yako ya Kuzaliwa.
Mwenyezi Mungu akupe maisha marefu na yenye furaha tele.

*Umetutupa waspmaji wa kazi zako!*

*Dec 31

Ukifanikiwa kutengeneza pesa nyingi usipandishe gharama za maisha yako.

-Juliana Isondo

**TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.**
**Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.**
**Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com**

JE MPYA UTATOBOA?

Mbili ziro mbili nne, mwaka umetukimbia
Meambulia unene, kazi ni nyama na bia
Usi-ku-cha kwa manane, kreti mbili metupia
Mwaka metukimbia, je mpya utatoboa?

Kujenga tajenga kesho, leo wacha nitumbue
Lete kuku mchemsho, jirani anitambue
Eti kwako kichekesho, acha mi nijirarue
Mwaka umetukimbia, je mpya utatoboa?

Mpya mwachie Mola, maisha yaishi leo
Mengine ni kombolela, teseka hupati cheo
Mambo hobela hobela, niacheni mwanaleo
Mwaka umetukimbia, je mpya utatoboa

Majuto ni mjukuu, wahenga walituasa
Hayawezi kutukuu, ya kale siyo ya sasa
Yatapokupata mkuu, utacheza kwasakwasa
Mwaka umetukimbia, je mpya utatoboa?

Mbili Ziro Mbili Tano, hiyo imetufikia
Maisha ni mapambano, ukizubaa jutia
Kila kitu mbanano, changa kaarata sawia
Mwaka umetukimbia, je mpya utatoboa?

Usipoishi kwa mipango, mendeleo tasikia
Wa mafaniko mlango, kamwe hutouingia
Utaishi kama Rango, wengine kuigizia
Mwaka umetukimbia, je mpya utatoboa?

Mwaka umetukimbia, je mpya utatoboa?
Mara mbili fikiria, nini kitachokutoa
kisha wekea nia, pambania tatoboa
Mwaka umetumbia, je mpya tatoboa?

Maisha si kukariri, mabadiliko muhimu
Kitaka nunua gari, kabla fikiri ya muhimu
Usijione tajiri, ukadharau walimu
Mwaka umetukimbia, je mpya tatoboa

Bidii ndiyo siri, ya mbali kutufikisha
Kitaka kuona mbali, jicho shuti kufikicha
Na tujitoe muhali, mwaka usije tuchosha
Mbili ziro mbili tano, piga hatua kiuchumi

**Na. Mbazi Mwanakwetu**
**Newala Mjini**

**MAISHA CHUNGU CHA MOTO**

Maisha chungu cha moto, kamwe usikipate
Maisha ni motomoto, upande au ukate
Maisha ni changamoto, ngumi au karate
Utachagua wewe…

Kuzaliwa hiari, kufariki ni lazima
Kwa masikini au tajiri, hiari ni yake mama
Kabla ye alifikiri, akuzae uwe wake mama
Jitafakari….

Acha yako jeuri, eti dunia twapita
Situletee mashairi, kwani waishi jupita
We umekariri, si ye hakuna kupita
Tupite twende wapi…

Mpaji ni Mola mmoja, mwenye mema dahari
Itakuja siku moja, si kwa shari bali kheri
Usikariri ngoja ngoja, subra huvuta kheri
Kwani we huogopi…

Kamwe sikate tamaa, yako njiani i yaja
Ni dhambi kata tamaa, yako ipo siku moja
Hata kama takataa,  imani ni jambo moja
Rafiki One day YES…


Sasa acha kubweteka, riziki haiji kwa upepo
Usijione umefika, kama aliyeonja pepo
Maisha mchaka mchaka, si kukemea mapepo
Pepo toka…

Anechumia juani, hukulia  kivulini
Walitwambia zamani, wazee wetu makini
Vipi kama u jangwani, chumo lako latakani
Changanya na zako….

Heshima kitu cha bure, zako ni zako mwenyewe
Mwenda si mkaa bure,  cha watu ni chao wenyewe
Halahala sisaure, heshima ni yako mwenyewe
Fanya kazi… tafuta pesa.

**Na. Shujaa Maneno**
**Bagamoyo — Pwani.**

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**




# OPERESHENI KASHMIR

Sasa Kinapatikana kwa Tsh

**15,000/=**

JIKAMATIE NAKALA YAKO

**DAR ES SALAAM**
**Duka la Kona ya Riwaya**
**Kinondoni Morocco**

**Simu: 0655428085**

Zammira

# KUTOKA MAKTABA: MAISHA NI MAPAMBANO—6

**Hiki ni kitabu kilichoandikwa miaka mingi sana nyuma. Kiliandikwa ili kiweze kusomwa na watu mbalimbali na kuwekwa kwenye maktaba za vijijini. Tunakitoa kutoka kwenye maktaba yetu ili kukupa uhondo, Ngurumo ya Mwandishi ni kisima cha fasihi chenye hazina iliyotukuka.**

## TAMAA YA UTAJIRI WA HARAKA HARAKA—6

Mradi mambo yalikuwa ya wasiwasi, waliokwenda kwa mganga walikwenda, walioamini mizimu nao walitambika na kadhalika.

Baada ya kufikihwa kituoni, Mpepo na rafiki yake waliulizwa maswali mengi. Mengine waliyajibu kwa busara sana kwamba, hata kama kungefunguliwa ukanda wa kunasa sauti wangeshangaa au kucheka.

Asakari: Wewe jina lako nani?
Luzolo: Mimi Luzolo, lingine Dhiki
Askari: Unakaa wapi?
Luzolo: Niko na Mpepo
Askari: Unakaa wapi, sikuulizi kama una pepo.
Luzolo: Ndiyo mzee kwetu Tetere kijijini.
Askari: Umefikaje huku Tunduma? Kwanza kufanya nini?
Luzolo: Tulikuja kwa mguu, tulian zia Mkuze kuchimba madini tukashindwa. Sasa tulikuwa tunajaribu hapa Tunduma.
Askari: Umekiri mwenyewe. Unajua ni kosa kuchimba madini bila kibali?
Luzolo: Siyo kosa, kwani si madini ya Mungu. ina maana hata nyasi tusikate kuezeka nyum ba?
Askari: Unahitaji kuelimishwa. Lakini bado una kosa. (akamgeukia mpepo) Na wewe jina lako nani?
Mpepo: Naitwa Mpepo tu.
Askari: Aaa, ndiyo maana awali Lu zolo alisema na pepo… ok.
Askari: Je, mambo yako ni sawa na mwenzio au wewe una lingine la kusema.
Mpepo: Hapana sisi sote njia yetu moja. Lakini naomba nipeleke salamu kwa mama Tabu kule Tetere. Nipeleke kwa simu ya upepo.
Askari: Sawa. Kumbe nyie wote mna pepo. Kosa lenu ni moja. Sasa nawafungulieni mashitaka katika vipengele vitatu vya sheria: kwanza kuchimba madini bila leseni; pili kuchimba se hemu isiyoruhusiwa na tatu kutaka kuiba mali asili ya serikali.

Mpepo: Bwana mkubwa mimi na taka kwenda nyumbani. Kazi hii siiwezi. Kwanza hatukupata chochote ad habu ya nini? Tuache twen de zetu Tetere.
Askari: Haya ingieni ndani maneno hayo mtamwambia hakimu kesho asubuhi saa mbili.

Lakini Mpepo na rafiki yake wakawa mahabusu usiku ule. Asubuhi askari alikwenda kuwachukua wahalifu hadi mahakamani. Kwa vile hawakuwa na mali yoyote, na pia kufuatana na maelezo yao, ambayo hawakuficha hata moja; hakimu aliwahurumia. Lakini sheria ni sheria. Pamoja na huruma, aliwahukumu kifungo cha miezi mitatu kila mmoja.

Baada ya kumaliza kifungo chao walitoka na kuelekea kwao Tetere mikono mitupu na huku wamechakaa vibaya sana. Walikumbuka tena maneno waliyopewa njiani na wasafiri wakati walipokuwa wanakwenda Tunduma.

Mpepo hadi leo hakubaliani na usemi kwamba 'penye nia pana njia'. Kila anaposimulia mikasa yake humalizia kwa maneno yafuatayo.

"Ikafika siku nilipokata tamaa kabisa ya kufanya kazi ile. Nikajitoa. Ingawa tulikuwa na nia, njia haikupatikana".

Mpepo alikaa nyumbani kwa muda wa miaka miwili bila mpango wowote maalumu. Lakini baada ya kutafakari kwa undani, pia kusongwa na maisha duni akaanza kujishughulisha na shughuli za maendeleo kijijini.

**Katika toleo lijalo tutaendelea na sehemua ya Tatu.**

SOMA VITABU

- Kwa afya ya ubongo wako
- Kwa kujiongezea maarifa
- Kwa burudani

USISITE

- Kumsimulia mwingine hadithi uliyosoma
- Kumfundisha mwingine yale uliyojifunza
- Kumshauri mwingine kitabu cha kusoma

NI VIZURI

- Kutembelea maktaba
- Maduka ya vita
- Kupiga stori na waandishi

# ELIMU JAMII

## USINGIZI

**Kwanini tunalala?**

Kupata muda wa kulala kidogo mara kwa mara ni vizuri kwa ubongo wetu na husaidia kuuweka ubongo kuwa mkubwa kwa muda mrefu, wanasema watafiti wa Chuo Kikuu cha London.

Watafiti hao wamebaini kuwa ubongo wa watu wanaopata muda kidogo wa kualala ulikuwa na sentimita za ujazo wa 15 sawa na inchi 0.9 na hali hiyo pia inachelewesha kuzeeka kwa kati ya miaka mitatu na sita.

Lakini, wanasayansi wanapendekeza kulala kwa chini ya nusu saa.

Wameongeza kuwa kwa wale wanaofanya kazi mchana, usingizi wao ni wa nadra sana kutokana na kubanwa na kazi nyingi, huku utamaduni wa kufanya kazi mara nyingi ukipinga suala zima la kulala mchana maeneo ya kazini.

"Tunapendekeza kwamba kila mtu anaweza kupata faida fulani kutokana na kulala," Daktari Victoria Garfield anasema. Alielezea matokeo hayo kama "riwaya kabisa na ya kusisimua kabisa".

Kulala usingizi kumeonekana kuwa muhimu kwa maendeleo ya ukuaji hasa kipindi cha utoto, na hali hiyo hupungua kwa kasi kubwa kwenye utu uzima sana kisha kupata umaarufu tena baada ya kustaafu, huku asilimia 27 ya watu walio na umri wa zaidi ya miaka 65 wakiripoti kupata usingizi wakati wa mchana.

Daktari Garfield anasema ushauri wa kulala usingizi ni "jambo rahisi sana" kwa kulinganisha na kupunguza uzito au mazoezi ambayo "ni kazi ngumu na hatua kubwa kwa watu wengi".

Ubongo kwa kawaida hupungua kwa umri, lakini ikiwa unapata usingizi unaweza kusaidia kuzuia magonjwa kama vile Alzheimers tatizo linalomfanya mtu kutoshiriki katika mazungumzo kwa muda mrefu, japo utafiti zaidi bado unahitajika.

Kwa ujumla afya ya ubongo ni muhimu kwa ajili ya kukulinda dhidi ya shida ya akili na hali hiyo inahusishwa na usingizi usio na wasiwasi.

Watafiti wanapendekeza kuwa tabia ya kutolala kwa wakati kunaathiri afya ya ubongo kwa kuathiri miunganisho kati ya seli za ubongo.

"Kwa hivyo, kulala mara kwa mara kunaweza kusaidia kukulinda dhidi ya kuzorota kwa mfumo wa neva kwa kufidia usingizi duni," mtafiti Valentina Paz alisema.

Hata hivyo, Daktari Garfield huwa hapendi sana kutafuta eneo zuri la kukalala mchana akiwa kazini lakini badala yake huwa anatumia njia mbadala za kutunza ubongo wake.

"Kusema kweli, ningependa kutumia dakika 30 kufanya mazoezi kuliko kulala, labda nitajaribu na kupendekeza kwamba mama yangu afanye hivyo."



### Jinsi ya kupata jibu?

Kusoma somo la usingizi kunaweza kuwa changamoto.

Kulala kunaweza kuimarisha afya, lakini kinyume chake pia ni kweli kwani afya yako inaweza kukuacha umechoka sana unahitaji kulala zaidi.

Kwa hivyo watafiti walitumia mbinu ya busara ili kudhibitisha kuwa kulala kuna faida.

Walitumia jaribio kubwa la asili kulingana na vinasaba vya kanuni ya maumbile ambayo tunazaliwa nayo. Tafiti za awali zimebainisha vijisehemu 97 vya vinasaba yetu

ambavyo vinatufanya tuwe na uwezekano mkubwa wa kuwa walala hoi au kuwa na nguvu siku nzima.

Kwa hivyo watafiti hao walichukua data kutoka kwa watu 35,000, wenye umri wa miaka 40 hadi 69, walioshiriki katika mradi wa Biobank wa Uingereza na kulinganisha kwa urahisi wale wanaolala na wale "wasiolala".

Matokeo, yaliyochapishwa katika jarida la Afya ya Kulala, yalionyesha tofauti ya sentimita 15 za ujazo sawa na miaka 2.6 hadi 6.5 ya uzee. Jumla ya ujazo wa ubongo ulikuwa takriban sentimita 1,480 za ujazo katika utafiti.

"Ninafurahiya kulala kwa muda mfupi wikendi na utafiti huu umenishawishi kwamba nisijisikie mvivu wa kulala, huenda hata unalinda ubongo wangu," Prof Tara Spires-Jones, kutoka Chuo Kikuu cha Edinburgh na rais wa British Neuroscience. Anasema

Alisema utafiti wa "kuvutia" wa matokeo ulionyesha "ongezeko ndogo lakini kubwa la ujazo wa ubongo" na "kuongeza kwa data inayoonyesha kuwa kulala ni muhimu kwa afya ya ubongo".

Watafiti hawakusoma moja kwa moja kuwa na usingizi mkubwa katikati ya mchana, lakini walisema sayansi ilielekeza kukatwa kwa nusu saa.

## Kwanini Tulale Usingizi?

- Usingizi ni mchakato muhimu unaoruhusu miili yetu kupumzika, kurekebisha, na kupona.
- Wakati wa kulala, miili yetu hurekebisha na kutengeneza upya tishu, kutia ndani moyo na mishipa ya damu.
- Usingizi una kazi muhimu katika ujumuishaji wa kumbukumbu na udhibiti wa hisia.
- Kupata usingizi wa mzuri wa kutosha ni muhimu kwa kudumisha afya mfumo wa kinga na kusaidia utendakazi bora wa ubongo.
- Usingizi husaidia kudhibiti hali yetu na kimetaboliki, ambayo inaweza kuwa na athari kubwa kwa uzito wetu na afya kwa ujumla.
- Kukosa usingizi kwa muda mrefu kuna hatari kubwa ya ugonjwa wa kisukari, fetma, ugonjwa wa moyo au kiharusi.
- Kukosa usingizi kunaweza pia kuathiri ustawi wetu wa kihisia, na kusababisha kuongezeka kwa matatizo na viwango vya wasiwasi.

**Sababu za kukosa usingizi**

- Kulala sana wakati wa mchana
- Kunywa kafeini (kwa mfano, kwenye soda, kahawa au chai) mchana au jioni
- Kutazama kipindi cha televisheni/filam ya kutisha kabla tu ya kulala
- Kufanya mazoezi ndani ya saa chache kabla ya kulala
- Msongo wa mawazo, mfadhaiko, au wasiwasi
- Usumbufu wa kimwili kutokana na matatizo ya afya au majeraha
- Matumizi ya dawa fulani au dawa za mitaani
- Kusinzia wakati wa mchana)
- Kubadilisha mara kwa mara zamu tofauti kazini
- Kusafiri kwenda kwenye eneo lenye muda tofauti
- Kukaa macho sana usiku
- Kupumua kwa shida wakati wa kulala

**Mwanadamu anatakiwa kulala usingizi kwa saa zisizopungua NANE. Je wewe unalala kwa saa ngapi ndani ya saa 24?**

*Imeandaliwa kwa msaada wa mtandao!*

# HAPPY NEW YEAR '02'—Twahir Yusuph

**Magari ya askari polisi yaliongezeka, jumla yakawa matano. Maafande wakalivaa jukumu la kumtuliza kiongozi wao, walimwinua na kumpakiza garini.**

***Endelea...***

Ni kwenye gari lake, askari waliobaki wakashughulika na zoezi la kuisitiri maiti hiyo iliyo kwenye kiroba, bila kusahau kisanduku kilichohifadhiwa kichwa chake. Muda huo kamera ziliruhusiwa. Ulikuwa msiba mzito mno kwa Edward, uliolisikitisha Taifa zima. Msiba ulioacha wingi wa maswali, ambayo wa kuyajibu ni aliyeusababisha tu, wanampata wapi sasa? Kwanza kwanini anajiamini hivyo? Aue, aoneshe, bado aje kuwaachia maiti yao karibu kabisa na makao yao makuu? Hapana, huyu lazima asakwe kivyovyote vile, na apatikane aeleze.

❣❣❣

Kwa namna alivyouliwa kinyama kijana Jax Edward Kituo, taratibu za mazishi yake zikapangwa zitamatishwe siku inayofuata asubuhi na mapema. Hapakukawia. Palikucha. Ulikuwa msiba mkubwa na tanzia kwa Taifa, viongozi takribani wote wa kiserikali walihudhuria nyumbani kwa mkuu wa jeshi la polisi. Hakukuwa hata na ibada ya kuaga. Isingewezekana kwa jinsi mwili wake ulivyoharibiwa. Jax alikuwa ndiyo mtoto aliyetarajiwa aje kusimamia kila anachomiliki mzee Edward Kituo, kati ya watoto watatu wa mzee huyo. Alimuandaa kwa ajili hiyo, lakini miaka 29 pekee ilitosha kwa yeye kuifurahia dunia hii aliyotenganishwa nayo kilazima.

Hii ilimuumiza baba yake. Alibaki na watoto wawili aliozaa na mkewe wa sasa, wote wa kike. Jesca ambaye ni mkubwa alikuwa na umri wa miaka 16, mdogo wake Jeniffer akiibeba 12 kwenye mifupa yake. Familia yote illikuwepo msibani hapo huku nyuso zao zikilowana huzuni tepetepe. Rais, waziri mkuu, hadi mkuu wa majeshi wote walihudhuria. Paji la Baba wa marehemu, IGP Edward kituo lilidhoofika kwa kilio, macho yake yalisadifu machungu ya huzuni iliyomkaanga haswa. Mama mzazi wa marehemu alishafariki miaka mingi iliyopita. Hakuwepo. Msiba uliendelea, ratiba zilifuatwa kama ilivyotakikana, hotuba za pole zilianza kunadiwa mazikoni hapo. Sasa ilifika zamu ya mkuu wa majeshi ya ulinzi na usalama nchini (CDF) Rashidi Koboko. Kabla hajazungumza machozi yalimlenga, hakuificha huzuni aliyonayo dhidi ya kifo hicho cha mtoto wa IGP Edward Kituo.

"Awali kabla ya yote, jeshi la polisi limeshatoa saa 48 huyu mnyama tayari awe ameshakamatwa, haiwezekani, haiwezekani, haiwezekani hata mara moja atutendee kitendo kama hichi na bado abaki uraiani akistarehe." akaweka tuo. "Jax alikuwa kama mtoto wangu wa kumzaa, nyumba yangu ilimzoea, familia yangu haikutimia kama nisingemuona yeye na ndugu yake Imraan" akaweka kituo kikuu kiongozi huyo wa majeshi bwana Rashidi Koboko.

Akaipa nafasi leso usoni pake, imfutie machozi yaliyoanza kumkosea adabu, kwa kumtoka bila ruhusa. "Mwanangu Imraan na yeye waliishi pamoja tangu watoto hadi wanakua wote, hata sisi wazazi wao ilikuwa hivyo, mimi na IGP Edward Kituo. Nasikitika sana kwa kifo alichouawa, muuaji ametuonesha roho chafu kiasi gani anayoimiliki, nasi tunasema hatutalivumilia hili. Lazima atafutwe na apatikane popote alipo, hata kama atajificha sehemu gani kwenye Dunia hii, tutampata tu." Aliweka tuo CDF Rashidi Koboko, huku safari hii akipangusa machozi mashavuni pake.

Waandishi wa habari mbalimbali walisheheni msibani hapo, kila tukio lilirushwa mubashara kupitia vituo vyao. Baadhi ya wananchi waliyafuatilia majumbani, na popote ambapo yalioneshwa. Watu wengi mashuhuri walihudhuria pia, akiwemo na mtoto wa mtu mzito nchini humo aliyeitwa Labi Kimati, mtoto wa mzee Kimati Sesewa, moja ya tajiri mwenye nguvu ndani ya Taifa lao la TAKASENI. Hotuba ya mkuu wa majeshi Rashidi Koboko ilipokuwa ikiendelea, Labi Kimati alikuwa makini kufuatilia, lakini punde akaitoa simu yake mfukoni na kuanza kuichezea. Muda huohuo akiwa anatoa hotuba simu yake CDF Rashidi Koboko ilikuwa ikiita mfukoni pia, aliweka mtetemo hivyo haikupiga kelele. Aliipuuza, dakika moja mbele simu ya Rais, Waziri Mkuu na mfiwa IGP Edward Kituo zote ziliingia jumbe kwa pamoja. Dakika hiyohiyo tena, kila mwandishi wa habari alionesha kuitazama simu yake, minong'ono iliyoambatana na miachamo ya midomo yao, ilishika kasi


msibani hapo.
Wengine walivishika vichwa vyao kwa mshangao, wengine walimtazama aliyekuwa akiwahotubia kwa jicho la masikitiko mno. CDF Rashidi Koboko aliona, alishuhudia sura za watu zinavyomtumbulia macho kwa mtindo tofauti na awali alipoanza kutoa hotuba hiyo ya pole. Kabla hajakipa hata swali moja kichwa chake ya nini kinachoendelea, simu yake ilikuwa ikitetema tena mfukoni. Hakuidharau dakika hii, aliichomoa na kushiriki kuitazama kama wengine wafanyavyo kwenye simu zao.
"Washa Data" jumbe ilieleza hivyo, kutoka namba ambayo haikuwepo simuni mwake, sababu ya kumjia bila jina. Ajiulize nini sasa? Wakati keshaambiwa cha kufanya. Haraka alitii kama jumbe hiyo ilivyomuamuru.

Kwa wacheza kamari, tunaweza sema ni sawa na chaguzi la timu zote kufungana, ila kwa kuwa ni msiba, basi tutaiita tanzia juu ya tanzia nyingine. Alistaajabu, mboni zilimsimama pima CDF Rashidi Koboko, ni kama jasho lilijibanza pahali, na sasa ilifika muda wake wa kujionesha, lilimchirizika likiwa jembamba mno, asijue hata limetokea wapi.
Kaona nini? Haraka akayatoa macho yake juu ya kioo cha simu yake aliyoitazama, kwa wasiwasi sana akawa anaangaza safu ya mbele waliyoketi viongozi wakubwa wa kiserikali, na hadi nyuma yake. Haikutosha, akawa anayageuza kila pande kuangaza, huku hofu ikimjaa..

Kimemkuta nini CDF? Punde akautupa mkono wake kifuani, bavu lake la kushoto, pahala moyo unapopumzika, huku akiyafinya macho yake kwa nguvu. Ni kama ulikuwa ukimuuma kwa namna sura yake ilivyokuwa imejikunja, pia akiugulia. Papohapo machozi yakaanza kumchapa vibao kwenye mashavu yake, haya sio kama yale ya mwanzo, yalizidi. "Imraan" aliita jina la mwanawe aliyetoka kumtaja muda mchache uliopita, ndio yule rafiki wa karibu na marehemu waliyehudhuria msiba wake huo unaoendelea. Wanajeshi wawili walisogea haraka hadi kwenye jukwaa hilo dogo alipokuwa akihotubia. Walimshika kiongozi wao aliyeanza kuliita jina la mwanawe mfululizo, "Imraan, Imraan, Imraaaan." alizidi kuliita, huku akilia kwa hasira chungu mno.

Huzuni juu ya huzuni, kioo cha simu yake alichokitazama dakika kadhaa zilizoondoka, kilibeba jina lilelile, KIFO. Kikiwa na video yenye maandishi yaleyale, HAPPY NEW YEAR kwa chini, tena mara hii ikiongezwa na "POLE BWANA RASHIDI KOBOKO, MKUU WA MAJESHI YA ULINZI NA USALAMA, ALIYESHINDWA KUILINDA DAMU YAKE MWENYEWE".

Pia ililionesha tukio lenye ukatili na unyama uliokithiri. Ni kama la jana tu, hili wanalolihudumu sasa kwa msiba. Leo lilitendeka kwenye roho na mwili wa Imraan, ni mwanawe wa pili kuzaliwa bwana Rashidi Koboko. Ni tukio baya mno, katikati ya siku mbaya sana kwao. Kwanini Imraan? Kwanini hawa watoto wa wenye madaraka mazito serikalini? Muuaji ana kusudio gani? Hayo ni maswali yaliyokuwa yakipita kwenye vichwa vya wanahabari, ila kwa muuaji huenda walistahili hukumu hiyo, kuwaua na kuwadhalilisha wengine wakiona. Ni msiba mwingine, katikati ya waliouhudhuria ambao hata marehemu wake hakusitiriwa kwenye hekalu lake la milele. Uzito wa simu ulivizidi viganja vyake, ilimdondoka bwana Rashidi Koboko aliye mikononi mwa askari jeshi wake, waliyemzuia asianguke. Mmoja wa askari jeshi hao aliiokota, lakini muda huohuo iliingia jumbe nyingine kwenye simu hiyo, Rashidi Koboko akaiomba simu yake aitazame, ni kheri hata asingefanya. ***Itaendelea...***



# "SHEMEJI USIZIME TAA...! NAOGOPA UKIMWI...! - 03

Na. G.K. Jr. Rogger Miller

**"No! Just a matter of time, una haki ya 'kumuaproach' binti yeyote. Kwa upande wangu sina chochote cha kukuambia, labda hapo baadae, tukijaliwa kuonana miaka ijayo"**
**Jibu lake lilinimaliza nguvu na nikahisi amechukia….**

Endelea…

"Sina uhakika kama nitakuona tena"
"He! D.K, labda usinitafute, tuombe uzima, halafu nishafika nyumbani dereva D.K, nyumba ninayokwenda ni ile pale yenye rangi nyekundu, penye geti jeusi" alisema huku akinieleza nyumba ile iliyokuwa mkabala na lango la kuingilia magari kwenye shule ya sekondari. Sikuamini tulifikaje mapema vile, wakati nilikuwa na mengi ya kulonga.

Nikatumia utaalamu na uzoefu kulizungusha gari, kisha nikapiga breki na kusimama.
"Ninatamani kukuona tena siku nyingine, lakini hapa naona ni geti kali, sina uhakika kama nitakuona tena!" nilisema kwa unyonge.
"Ukija hapa, nenda pale pembeni kwenye ile salon, pale! Ukiingia ulizia binti mmoja anaitwa Hilda. Ukimpata Hilda, umenipata," alisema, na kwa mara nyingine tena, macho yake mang'avu hata gizani, yaliuchoma moyo wangu. Nilitingisha kichwa kukubaliana na maelezo yake.
"Asanteni sana kwa kunileta, nashukuru na kwaherini… safari njema," alisema huku akifungua mlango na kuanza kushuka loooh...! Wakati anashuka, sketi yake iliyaacha tena wazi mapaja yake mazuri, nikapatwa na mfadhaiko. Hakujali, alishuka na aligeuka kunipungia mkono. Alianza kuondoka kwa hatua za taratibu, na kwa msaada wa taa za gari, mwendo wake ulinitesa, kwani ulikuwa ukiyayumbisha maungo yaake ya nyuma yaliyonona kiuchokozi nikabakia nimeduwaa na kumeza mate.

"Oyaa dereva, unalemaa nini, demu ulikuwa naye humu ndani, umeshindwa kuzoza naye, usiku unauweka, rusha mashine suka" kondakta wangu alinishtua toka kwenye mawazo ndipo akili yangu ikarudia hali ya kawaida, nikapiga kiti na kuondoa gari. Niliendesha gari taratibu, na mawazoni mwangu palijaa umbo la Ray pamoja na harufu aliyoniachia ambayo sikutaka iishe upesi.

Baada ya siku mbili, siku ambayo nilikuwa 'off' niliamua kwenda Mabibo-Royola kujaribu kumpata Ray. Siku hiyo nilikwenda na gari ndogo aina ya Toyota Chaser 'Mayai'. Nilikuwa naenda kubahatisha tu, kwani sikuwa na uhakika kama maelekezo ya Ray yalikuwa sawasawa. Niliegesha gari nikashuka kuelekea kwenye salon ambayo nilielekezwa.
Nilisukuma mlango wa kioo, nikajitoma ndani na kukutanisha macho yangu na mabinti wawili wachangamfu. Uvaaji wao ulikuwa ni matunda ya Tamthiliya ya ACAPULCO BAY na sura zao zenye mvuto zilinipagawisha. Nikawasabahi na kuketi kwenye moja ya makochi mazuri yaliyokuwa pale ndani. Bila kupoteza muda niliowauliza kati yao Hilda alikuwa yupi. Nikamuona mmoja wao akitabasamu, meno yake yalionesha kutunzwa vyema, bila shaka na 'Close Up'.
"Ni mimi, nikusaidie nini anko" sauti yake ilikuwa tamu kushinda ya yule sister du 'bishoo' wa Radio fulani.
"Sawa, ninaitwa D.K au don na shida yangu ni kuonana na Rehema au Ray"
"Anhaa ametoka kidogo, kaenda MCA Pub, kuna shughuli ya dharula pale. Kama una shida kubwa sana ambayo sisi hatuwezi kuitatua, nitakupeleka" binti yule, Hilda, alisema huku akiyazungusha macho yake na kuvuta kivazi chake cha juu ili kufunika tumbo na kiuno chake, ambavyo vilikuwa ….. Yaani we acha tu. Ati kama nina shida ambayo wao hawawezi kuitatua! Mungu wangu! Hivi hawa mabinti walikuwa wanajua kwa nini namsaka Ray? Laity wangejua kuwa shida yangu ni mapenzi, wasingethubutu kusema vile, ole wao!
"Labda aliacha ujumbe wowote" niliuliza baada ya kutafakari kwa muda.
"Kwa leo hakuacha, ila alisema siku mbili zilizopita, kuwa kuna mtu anaitwa D.K akija kumuulizia, kama atakuwa karibu tumwite" Hilda aliongea kwa sauti ambayo nilitamani kuila na kuimeza. Nikatingisha kichwa.
"MCA Pub unapafahamu?" alinihoji huku akiwa amenikazia macho yake malegevu. Nilikuwa na-

pafahamu vyema, lakini kwa kutaka kuzoeana na binti yule, na ili niweze kumzozea sera zangu, atakapokubali kunipeleka, nilikataa, nikamwoma anipeleke. Mawazoni mwangu kulishajengeka picha ya kugeuza kibao na "kumuaproach" Hilda, kwani alikuwa demu moto si mchezo. Alinichota kuliko Ray, ingawa Ray nilimuona us-iku. Kilichonivutia ni jinsi Hilda alivyokuwa na "tuta" la nguvu, na miguu iliyononа (na hayo ndiyo maradhi yangu, kama dokta fulani na binti…) kwa kweli hawa watu, Hilda na Ray, walikuwa wamebarikiwa na kupendelewa "kujazia" ile kisawasawa. Nikahisi kama siyo Wanyamwe-zi basi Wahehe au Wasukuma (habari hii kwa wengi ni ngeni… basi jueni hivyo) lakini kwangu miye ni common. Hilda alinikubalia kunipeleka, tukafuatana naye hadi "Chaser" ilipokuwa na kuzama ndani.
Nilipoondoa gari, nilianza biashara mara moja, lakini ni-kapoza moto na kumkumbuka Ray. Kama Ray angekuwa hana haja name hasingeacha maagizo. Kwa hiyo nikajua kuwa alikuwa ameingia 'line' na nilikuwa na kazi ndogo tu ya kumalizia.
Hilda, niliykuwa naye garini alichota akili yangu kwa pa-senti kubwa. Kama ningefanya papara kutangaza sera, pengine ni mdogo wake, si nitakosa vyote! Nikazidi ku-tulia na kutafakari upya tamaa yangu.
"Hilda, wewe na Ray mkoje, yaani ni nani kwako?"
"Mimi na Ray ni mtu na binamu. Yeye ni mtoto wa shangazi name ni mtoto wa mjomba wake, umenipata?" Hilda alinifahamisha, nikatingisha kichwa kukubaliana naye na nikamuuliza tena.
"Ile salon ni ya kwako?"
"Hapana, ni ya mama, ila pale mimi ndiye mtaalamu, ulipoingia miye nilijua umekuja kuweka "wave".
"Siku nyingine nitakuja kwa ajili hiyo" nilimjibu na kushangaa kuwa tumeshafika maeneo ya SNAKE GAR-DEN, karibu kabisa na MCA Pub.
"Hilda, umeolewa au umeshachumbiwa"
"Mbona unaniuliza hivyo!" alimaka na kukizia macho, ni-katabasamu na kumkonyeza, akacheka na kunionesha kidole kama aliyekuwa akinionya.

***Itaendelea toleo lijalo...***

**ANDIKO NYETI**

VIRGINIA HALL - MWANAMKE ASIYE NA UMUHIMU

Virginia Hall ni mmoja kati ya majasusi muhimu sana wa Marekani ambaye hakuwahi kusikika.
Simulizi yake inapatikana kwenye bango la onesho ndani ya Makumbusho ya CIA yaliyopo kwenye Makao makuu ya CIA huko Langley, Va.— lakini haikuwa kwa ajili ya kila mtu.

"Alikuwa ni mwanamke mwenye kujipamba sana wakati wa Vita ya Pili ya Dunia," anasema Janelle Neises, mku-rugenzi msaidizi, anayesimamia makumbusho hayo. Kwanini watu zaidi hawajasikia kuhusu Hall? Nukuu kutoka kwenye maandishi yake ya kijasusi inatoa maelezo juu ya hili: "Marafiki zangu wengi waliuawa kwa kuwa walikuwa wanaongea sana."

Lakini sasa – zaidi ya miaka 70 baada ya mlipuko wa vita huko Ufaransa, na baada ya takribani miaka 40 baada ya kifo chake – Virginia Hall anapata nafasi. Vitabu vitatu vimechapwa. Filamu mbili zinatengenezwa. Mwandishi wa vitabu wa Uingereza Sonia Purnell ameandika moja ya vitabu hivyo, Mwanamke Asiye na Umuhimu, na amemkejeli kwenye kichwa cha wasifu wake "Pamoja na mengi ya maisha yake, maisha yake ya awali, alikataliwa na kudharauliwa " ameandika Purnell. "daima amekuwa akifukuzwa ama kupuuzwa kama mtu ambaye si muhimu au hana umuhimu."

Hall alizaliwa kwenye familia ya kitajiri ya Baltimore mwaka 1906, malezi yake yalimfanya aolewe na yule ampendae. Lakini alitaka zaidi matukio ya hatari. Ali-penda kujiita "asiyebadilika na wa kuogofya." Alipenda kuwinda. Mara moja aliwahi kwenda shule akiwa na kem-be lililotengenezwa kwa nyoka walio hai.

**Elimu Ufaransa**

Kwa kifupi, Hall amesoma katika Chuo cha Radcliffe na Barnard. Halafu akaenda kusoma huko Paris na kujikuta akiipenda Ufaransa. Purnell anasema, Hall aliamua kuwa mwanadiplomasia.
"Alitaka kuwa balozi. Aliwekwa pembeni na idara za kiserikali. Aliomba mara nyingi," anasema Purnell.
Hall alifanya kazi ya ukarani wa ardhi katika ubalozi mdogo wa Marekani nchini Uturuki. Lakini wakati aki-winda ndege, alijifyatulia risasi mguuni kwa bahati mbaya. Akapata donda ndugu, hivyo mguu wake ukakatwa kuanzia chini ya goti.

***Mwendelezo utaukuta toleo lijalo….***

# TANGAZA NASI HAPA KWA 10,000/= KWA MATOLEO MAWILI

## Tupate:

**Email: jamvilasimulizi@gmail.com**

**Whatsapp: 0766974865**


Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi
jamvilasimulizi@gmail.com